# Nipashe

Jumanne Juni 2, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580247

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Sirro: Hatutatumia bunduki kutisha watu uchaguzi mkuu

UK. 2



Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Kasa kutamia, ngadu mitini, ni maajabu hifadhi baharini

ELIMU
NA MICHAEL ENEZA

Kupeana nafasi wangapi watarudi kwa mwaka au watasomea wapi?

UKURASA 11

## BAA LA CORONA



Kujilinda wewe na wenzako dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona ni muhimu kila wakati kuweka mikono yako safi kama inavyoshauriwa na watalaam wa afya..

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

# Waziri: Wagonjwa corona wamebaki 4

**Ni** Dar na Pwani, asema katika uwaziri wake hajawahi kupitia kipindi kigumu kama cha corona...

*Endelea UK. 2*



Mwalimu wa Taaluma, Liberatus Ntilema, akikagua wanafunzi wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Dodoma, walioanza masomo jana, huku walimu na wanafunzi wakichukua tahadhari zote za kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa corona. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


## WANAFUNZI WAREJEA, UONGOZI WAELEZA MIKAKATI

UKURASA 4

## PM ashangaa jengo la serikali kuuzwa mil. 40/-

UK. 2

**MICHEZO** KIKWETE ACHAMBUA MABADILIKO YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# IGP Sirro: Hatutaruhusu mtu kucheza na bunduki kutisha Watanzania

**Na Mwandishi wetu**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Saimon Sirro, amesema atahakikisha uchaguzi unafanyika kwa hali ya amani na utulivu na kutoruhusu mtu yeyote kucheza na bunduki kuwatisha Watanzania.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na askari wa mikoa ya Tabora na Singida, alisema jeshi hilo lina wajibu mkubwa kwenye uchaguzi mkuu.

Uchaguzi Mkuu unatarajia kufanyika Oktoba mwaka huu, na tayari maandalizi yameanza kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), kuandaa maadili ya uchaguzi yaliyopitishwa na wadau na kuchapishwa katika gazeti la serikali.

"Tunajiandaa na uchaguzi kila mtu atimize wajibu wake, tutahakisha uchaguzi unakwenda salama, unakuwa salama na amani, wale wachache wanaotaka kuvuruga tuwashughulikie kwa mujibu wa sheria," alisema.

IGP Sirro aliwataka askari kutoruhusu mtu yeyote kucheza na bunduki kuwatisha Watanzania

Aliwapongeza askari wa Mkoa wa Tabora kwa kazi nzuri na kwamba Mungu atawabariki kwa kufanya mkoa huo kuendelea kuwa shwari kutokana kujali kazi yao.

"Tunataka Tanzania habari ya unyang'anyi kwa kutumia bunduki iwe ni historia, nimekwenda Uganda habari ya bundunki haipo, kwa hiyo na sisi tufike mahali tuseme basi na iwe basi," alisisitiza.

"Niwatake askari wenzangu kwamba hatuna huruma na mtu wa namna hiyo na ndiyo njia pekee ya kuleta heshima ya Jeshi la Polisi...lina miaka 100 kwa sasa...mhakikishe watu wa Tabora wanaishi kwa amani."

Vile vile, IGP Sirro aliwataka askari wasiwe kero kwa wananchi wanaotii sheria na badala yake wawe mwiba kwa wasiotaka kufuata sheria.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na shtaka moja la kutoa rushwa ya Sh. milioni 10, ili kumpatia askari polisi Meshack Laizer aliyekuwa amewakamata wafanyakazi wawili wa kampuni ya Oryx wakiuza mafuta uchochoroni Moshono kinyume cha sheria ili waachiwe.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akizindua jengo la Mamlaka ya Bodi ya Mkonge Tanzania mkoani Tanga jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela. **PICHA: OSCAR KASIMIR**I.

# Dar, Pwani zabaki na wagonjwa corona 4

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema wagonjwa wa corona wamebakia wanne katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Alitaja idadi ya wagonjwa katika kila kituo kwenye mabano kuwa ni Amana (3) na Mlonganzira (1).

Kadhalika majiji ya Tanga na Mwanza, vituo vilivyotengwa havina wagonjwa.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana mbele ya Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, aliyeko ziarani mkoani Tanga kukagua shughuli za maendeleo ikiwamo kuzindua jengo la mkonge Tanga. Alisema katika uwaziri wake hajawahi kupitia kipindi kigumu kama cha corona kwa kuwa amehenya.

"Corona bado ipo tuendelee kuchukua tahadhari, tuendelee kujikinga...Nawashukuru viongozi wa dini, corona tumeishinda Tanzania, nikiangalia wenzangu kwenye nchi nyingine haki ya Mungu tunasema Mwenyezi Mungu nini hasa zaidi ya kumwambia asante kwa kutoa," alisisitiza.

Kuhusu corona, Waziri Mkuu aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa wanapokuwa kwenye mikusanyiko ili kujikinga na virusi.

# PM ashangaa jengo la serikali kuuzwa mil. 40/-

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameonyesha kushangazwa na kitendo cha jengo la serikali kuuzwa kwa bei ya kutupa ya Sh. milioni 40 kwa watu binafsi, hali iliyosababisha Bodi ya Mkonge nchini (TSB) kukosa jango la ofisi.

Majaliwa alionyesha kushangazwa na kitendo hicho jana wakati akizungumza na watumishi na wakulima wa mkonge kutoka mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani na Kilimanjaro kwenye ziara yake ya siku moja mkoani hapa.

Alisema serikali imepanga kurejesha mali za umma ili kurudisha imani kwa wakulima na wananchi, na kuendelea:

"Haiwezekani majengo haya yakauzwa milioni 40, halafu sio keshi hivi inaingia akilini kweli... majengo haya yapo katikati ya jiji, ukihoji unaambiwa serikali inatuonea."

Aliongeza kuwa mchakato wa urejeshwaji wa mali za umma hakuna mtu atakayependa.

"Katika zoezi hili hatumwonei mtu yeyote, nataka watu wajue hivyo na kwenye mikoa mitano tumefanya hivyo, hatujasikia malalamiko, leo tupo Tanga tunasikia kelele nyingi, hakuna mtu ambaye ataonewa," alisema.

"Leo nimepita huko pembeni mwa mji kwenye mikoko ndio naambiwa ofisi za bodi zilikuwa huko, sasa mali imereshwa kwenu," aliongeza.

Katika hatua nyengine, serikali imerasimisha timu iliyokuwa ikisaidia upatikanaji wa mali za Mamlaka ya Mkonge Tanzania mkoani Tanga na kuwa wajumbe kamili wa bodi ya mamlaka hiyo ili waweze kufanya maamuzi kamili ya kisheria.

Bodi hiyo ilirasimishwa na Majaliwa wakati akizindua jengo la Bodi ya Mkonge lililokuwa limeuzwa na kutumika kinyume cha taratibu na watu binafsi.

Waziri Mkuu aliwataka wakuu wa wilaya zote nchini ambao maeneo yao yanalimwa mkonge kuhakikisha maofisa kilimo wa halmashauri hizo wanakwenda kuwasaidia wakulima badala ya kukaa maofisini.

Alisema ni jukumu la wakuu wa wilaya wote kuhakikisha wanawaondoa maofisini na kuwapeleka vijijini maofisa kilimo wote ili wakawasaidie wakulima namna ya upandaji bora wa mkonge, na kukifanya kilimo kiwe na tija, kwani serikali imedhamiria kurejesha zao hilo katika thamani yake ya awali.

"Wakulima jipangeni kwenda kulima mkonge, zao hili sasa tumedhamiria kulirejesha katika thamani yake... wakuu wa wilaya endeleeni na hamasa kuhakikisha mkonge unarudi... tunataka tuone kila tunapopita mashamba ya mkonge nisisikie mkulima akilalamika, wapeni mbinu bora za ulimaji wa zao hilo," alisisitiza.

Aliongeza kuwa serikali itawapa msaada wakulima kuanzia wadogo, wakati na wakubwa.

"Tunataka kuona wakulima wakiongezeka kadiri wanavyoweza, Mkuu wa Mkoa ukipata mwekezaji popote ndani au nje wasaidiwe na walime ili kilimo kiwe na tija," alisema.

"Tunataka kuona wakulima wakiongezeka kadiri wanavyoweza, Mkuu wa Mkoa ukipata mwekezaji popote ndani au nje wasaidiwe na walime ili kilimo kiwe na tija," alielekeza.

Naye, Naibu Waziri Kilimo, Omar Mgumba, alimshukuru Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa anazozifanya katika kusimamia sekta ya kilimo likiwamo zao la mkonge.

"Uadilifu wako na uzalendo wako ulikufanya uunde kamati ya kuchunguza mali za Bodi ya Mkonge Tanzania na leo hii mali zao zimerudi."

"Mheshimiwa Waziri Mkuu utaingizwa kwenye kumbukumbu za Tanzania kwa kujitoa kwako katika kuhakikisha zao hili linarudi kama ilivyokuwa awali. Tutafufuka katika mikoa yote ambayo imeonesha inaweza kulima zao hili la mkonge, lengo ni kuhakikisha zao hili linarudi kwenye hadhi yake."

HABARI KITAIFA

# Kisutu yaibua kesi ya Lissu tuhuma uchochezi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana imetaja kesi inayomkabili aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, dhidi ya maneno ya uchochezi yenye lengo la kujenga chuki kwa wananchi kwa Rais John Magufuli.

Kesi hiyo iliyosajiliwa 279/2016, imetajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na upande wa Jamhuri umeomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hata hivyo, alidai kuwa mshtakiwa alijidhamini mwenyewe katika kesi hiyo.

Lissu alifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza katika kesi hiyo Agosti 6, 2016 na alisomewa mashtaka matatu ya uchochezi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Cyprian Mkeha (kwa sasa Jaji wa Mahakama Kuu).

Kesi hiyo ni ya tatu kati ya kesi nne za uchochezi zinazomkabili katika mahakama hiyo.

Awali, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi akisaidiwa na Paul Kadushi na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Kishenyi Mutalemwa, ulimsomea mashtaka yake mbele Hakimu Mkeha.

Kadushi alidai kuwa Agosti 2, 2016, katika viwanja vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Ilala, Dar es Salaam akiwa na nia ya kujenga chuki kwa wananchi dhidi ya Rais na serikali, alitoa maneno ya uchochezi na kunukuliwa: "Ukitaka kujua Magufuli ni dikteta uchwara ni pamoja na kauli zake." Alidai siku hiyo kwa nia ya kuleta dharau katika mfumo wa utoaji haki ndani ya mahakama na kuidharau alitoa maneno ya uchochezi kwa kwamba: "Kesi na mashtaka yenyewe ni ya kipuuzi na ya Kimagufuli gufuli."

Vile vile, inadaiwa siku hiyo kulikuwa na mwenendo wa kesi mbili za jinai ambazo zilikuwa zimekwishamalizika na alitoa maneno akiwa na lengo la kudharau mienendo ya mahakama.

Alinukuliwa: "Siwezi kufungwa, kesi na mashtaka yenyewe ni ya kipuuzi na ni ya Kimagufuli".

Upande wa Jamhuri ulipinga dhamana kwa madai kuwa ataingilia upelelezi.

Hata hivyo, jopo la mawakili tisa likiongozwa na Peter Kibatala, lilipinga hoja za Jamhuri kuzuia dhamana ya mshtakiwa kwamba anafahamika kuwa ni mbunge na dhamana ni haki yake.

Hakimu Mkeha alimtaka mshtakiwa kujidhamini mwenyewe.

Jana, Hakimu Isaya alipanga kesi hiyo kutajwa tena Julai mosi, mwaka huu.

# Watumishi watatu h'shauri wafukuzwa utovu nidhamu

**Na Allan Masele, SIKONGE**

WATUMISHI watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, mkoani Tabora wamefukuzwa kazi kwa tuhuma za utovu wa nidhamu na matumizi mabaya ya fedha za makusanya ya mapato ya ndani na kushindwa kuwasilisha serikalini.

Pia, watumishi wengine wameshushwa vyeo, kusitishiwa mikataba ya ajira na kusimamishwa kazi kwa ajili ya uchunguzi.

Akitoa taarifa ya uamuzi huo mbele ya wajumbe wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Peter Nzalalila, alisema watumishi hao wamefukuzwa na wengine kuchukuliwa hatua za kinidhamu kutokana na kukiuka maadili ya utumishi wa umma pamoja na misingi ya utawala bora.

Alisema uamuzi huo umefanywa kutokana na mapendekezo ya kikao cha Kamati ya Fedha, Mipango na Uongozi kilichoketi Mei 18, 2020 na kujadili tuhuma mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili watumishi hao na hatua zinazostahili kuchukuliwa baada ya kuitwa na kuhojiwa.

Aliwataja waliofukuzwa kuwa ni Jacob Chapaulinge (Mtendaji wa Kata), Donald Lyoba (Mtendaji wa Kijiji) na Elia Kaugila (Mtendaji wa Kijiji), huku Sabina Mhaya (Mtendaji Kata ya Ngoywa) akipewa onyo na kuwekwa chini ya uangalizi kwa miezi sita na kukatwa asilimia 15 ya mshahara kwa kipindi cha miaka mitatu.

Nzalalila alibainisha watumishi waliochukuliwa hatua za kinidhamu kwa kusitishiwa mikataba yao ya ajira kuwa ni Simon Michael Nonga, Rashid Bakari Namalembo, Charles Henry Kaswiza, Mipawa Jilala Kamuga na Nigangwa Baruga wote walikuwa madereva.

Alitaja watumishi waliovuliwa madaraka ya ukuu wa shule kwa tuhuma za kushindwa kusimamia miradi katika maeneo yao kuwa ni Baraka Lyandala aliyekuwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Majojoro na Mandi Nghulingi, aliyekuwa Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Kiloleni.

Vile vile, Mapambano Masota alivuliwa nafasi ya Kaimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Kilumbi, Mtendaji wa Kijiji cha Kiyombo, Wistone Ikanga, alisimamishwa kazi kupisha uchunguzi, huku Ofisa Elimu Msingi wa wilaya hiyo, Suzana Makoye na Ofisa Elimu Kata ya Kilumbi, Magesa Keneja wakipewa onyo la kwanza.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Tito Luchagula, alisema adhabu hizo ni sahihi kwa kuwa watumishi hao walienda kinyume na maadili ya utumishi wa umma ikiwamo vitendo vya utovu wa nidhamu na ubadhirifu.


TRA
MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

**TAREHE YA MWISHO YA KUWASILISHA RITANI YA MAPATO NA KULIPA KODI YA MAPATO**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha walipakodi wote kuwa tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Ritani za kodi ya Mapato na kulipa kodi kwa mwaka wa mapato unaoishia Disemba 2019 na wale wanaokadiriwa na kulipa kodi zao kwa awamu ni 30 Juni, 2020.

**ZINGATIA:**
Ili kuepuka usumbufu na misongamamono katika ofisi za TRA, walipakodi wote wanashauriwa kulipa kodi husika kabla au mnamo tarehe ya 30, Juni, 2020.

Riba na adhabu vitatozwa kwa mlipakodi yeyote ambaye hatazingatia muda unaotakiwa kulipa kodi kwa mujibu wa sheria.

Aidha tunakumbusha wale wote wenye madeni ya kodi kulipa madeni hayo ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Limetolewa na:**
**Idara ya Huduma na Elimu kwa Mlipakodi**

**Kwa mawasiliano zaidi piga simu**
**0080 750075; 0080 780078 au**
**tuma barua pepe kwenye**
**huduma@tra.go.tz**

# Wanafunzi warejea vyuo, shule kwa tahadhari

**Na Waandishi Wetu**

WANAVYUO na wanafunzi wa kidato cha sita jana wamerejea vyuoni huku kila taasisi ikiwa na mikakati ya kuhakikisha wanasoma na kufundisha kwa tahadhari kubwa dhidi ya corona.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakuu wa vyuo na shule hizo walieleza kuwa maandalizi ya kuhakikisha tahadhari zinachukuliwa yalianza mapema kutokana na ushirikishwaji uliofanywa na serikali.

Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni kila anayeingia ananawa mikono, anavaa barakoa na kupimwa joto la mwili, huku kukiwa na umbali wa mita moja kutoka mtu na mtu.

**TUDARCo**

Kaimu Mkuu wa Chuo Kikuu Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo), Prof. Andrew Mollel, alisema asilimia 70 ya wanafunzi wameripoti chuoni, na tayari marekebisho ya ratiba yamefanyika kuhakikisha masomo yaliyokuwa yafundishwe kwa wiki 17 yanafundishwa kwa kiwango na ubora ndani ya wiki 12 na baadaye wiki mbili za mitihani.

Alisema madarasani wanafunzi wanakaa umbali wa mita moja, na muda wa masomo utakuwa kuanzia saa moja asubuhi hadi saa 12 jioni, kwa kuwa na wanafunzi wachache.

"Tunawafanya wanafunzi wetu kutambua kuwa muhula huu ni mfupi na wajipange kupokea mafunzo kwa muundo tofauti ikiwamo matumizi ya teknolojia, pia tutafuatilia hosteli kuhakikisha wako salama," alisema.

Prof. Mollel alisema kwa kushirikiana na wataalam wa afya, wamewafundisha watumishi namna ya kujikinga, na yatakuwa endelevu kwa wanachuo wote kwa wiki ya kwanza.

"Tumeunda kamati maalum ya ufuatiliaji na kukishauri chuo kwa masuala hayo, tuna matangi ya lita 1,000 yenye koki mbili za kunawa bila kushika yapo kwa wingi, lazima upimwe joto kabla ya kuingia chuoni,"alibainisha.

Pia, kimeandaliwa chumba maalum cha kuwapumzisha wanafunzi watakaohisiwa kuwa na tatizo la kiafya huku wakiendelea kuangaliwa kabla ya kufikishwa kwa wataalamu wa afya.

**UDSM**

Ofisa Uhusiano wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Jackson Isdory, alisema idadi ya wanafunzi waliofika chuoni imeongezeka tofauti na siku mbili zilizopita.

**IFM**

Katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), wanafunzi walionekana wakiwa wamepanga mistari kwa kuachiana umbali kwa ajili ya kunawa mikono kabla ya kuingia ndani huku wamevalia barakoa.

**St JOHN**

Chuo cha St. John na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), wanafunzi waliingia wakiwa wamevaa barakoa, kupimwa joto na kutakasa mikono huku wamevaa vitambulisho.



Wanafunzi wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), wakiwa darasani kuendelea na masomo chuoni jana, baada ya serikali kuvifungua vyuo nchini kote kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona. **PICHA: JUMANNE JUMA**

Mmoja wa wanafunzi, Juma Abubakari, aliishukuru serikali kwa kudhibiti maambukizo ya ugonjwa huo na wanaamini watasoma katika mazingira salama.

Pia, Mwanafunzi wa mwaka wa tatu, Damas Kisamalala, alisema wanatarajia kufanya mitihani yao vizuri bila hofu.

**CBE**

Wakizungumza na Nipashe, baadhi wa wanafunzi wa Chuo cha Biashara (CBE), tawi la Dodoma (CBE), walisema takribani wote wameripoti kuanza rasmi masomo ambayo ratiba imeanza rasmi jana serikali ilivyotangaza.

Ally Mustapha, alisema wameanza masomo rasmi, kabla ya kuingia eneo la chuo na darasani kuna za maji kwa ajili ya kunawa mikono.

**UDOM**

Akizungumza na waandishi wa habari, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Profesa Faustian Bee, alisema hadi jana asubuhi, wanafunzi 12,533 walikamilisha taratibu za usajili na wengine wanaendelea kujiandikisha.

"Idadi siyo ndogo tuliwaelekeza waanze kujisajili tangu Ijumaa ya wiki iliyopita, inawezekana kuwa wengi wamefika Jumapili na leo (jana) ndio wameanza kujiandikisha kwa upande wetu tataendelea na usajili kila ambaye hajafanya afanye nina uhakika mpaka Ijumaa tutakuwa tumekamilisha," alisema Profesa Bee.

**SHULE YA DODOM**

Wanafunzi wote 214 wa kidato cha sita wameripoti na wameanza masomo kwa ajili ya kujiandaa na mitihani ya kitaifa itakayofanyika mwezi huu.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Ester Simchimba, alisema tayari wanafunzi hao wameripoti na kuanza masomo yao na tahadhari zote zimechukuliwa na wanafunzi na walimu ni lazima kuvaa barakoa na kupimwa joto wanapoingia darasani.

Kuhusu utaratibu wa wanafunzi kukaa, alisema darasa lililokuwa la wastani wa wanafunzi 71 kwasasa ni 38.

Alisema shule hiyo wamejipanga vizuri kuwafundisha wanafunzi kwa kila mwalimu kufundisha vipindi vyake wakati wa ziada ili kufidia vipindi vya siku za nyuma.

**MAVUNDE AKABIDHI VIFAA**

Katika hatua nyingine, Mbunge wa Dodoma Mjini na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Anthony Mavunde, amegawa vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo kwa shule zote za serikali na binafsi katika jimbo lake.

Alisema lengo ni kuhakikisha wanafunzi wanakaa kwenye mazingira salama na kuwaomba wa kidato cha sita kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo.

**MOROGORO**

Nipashe ilitembelea baadhi ya vyuo mkoani humo na kukuta wameanza masomo huku wakishauri Taasisi ya Utafiti ya Taifa ya Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kuzalisha kwa wingi na kwa gharama nafuu tiba lishe.

**SUA**

Prof. Raphael Chibunda, alisema kwa kutambua thamani ya lishe bora wanazalisha mchanganyiko wa lishe muhimu zitakazosaidia wanajumuiya wakiwamo wanafunzi na wananchi kwa ujumla.

"Hatutegemei kuwaambia wanafunzi waje na tangawizi, malimao, machenza au nini sisi, au waje na hela mahususi ya kununua hivi vitu, vyote tunazalisha na vinapatikana hapa hapa chuoni, hata ukienda kwenye duka letu la bidhaa za mboga utavikuta," alisema.

**MZUMBE**

Kaimu Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Mawasiliano, Rose Mdami, alisema: "Mzumbe kupitia kituo chake cha afya, tumeandaa wataalam wa kutosha ambao watakuwa wakitoa elimu mara kwa mara, kadhalika wakifuatilia kwa karibu afya za wanafunzi,ili inapotokea kuna tatizo lolote wachukue hatua za haraka na za makusudi."

Baadhi ya wanafunzi, Hassan Salim na Eline Goodlucky, walisema:

"Wanafunzi tumekatazwa kwenda na Spirit kwasababu ile ni rahisi kulipuka, lakini sanitaiza nyingine tumebeba na barakoa tayari ninazo tano, naamini hizi zitanisaidia kwa wakati wote wa masomo,"alisema Eline.

Kaimu Mkurugenzi wa huduma za afya, Mzumbe, Dk.Pachal Songoro, alisema tahadhari za kiafya zilizochukuliwa ikiwamo kutumia mitandao ya kijamii ya chuoni kwa wanaohisiwa kuwa na corona.

**PWANI**

MKURUGENZI wa Mafunzo wa chuo Cha Njuweni Kibaha Salma Mfinanga amesema vipindi vya darasani kwa wanafunzi vitafanywa kwa kufuata muongozo wa Wizara ya Elimu katika kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Corona.

Salma akiongea na Nipashe jana, alibainisha kuwa muda wa vipindi kwa siku utaongezwa lakini pia baadae siku za jumamosi wanafunzi wanaweza kuendelea na masomo kufidia muda wa ambao hawakuwa chuoni.

***Imeandaliwa na Salome Kitomari na Romana Malya (DAR), Paul Mabeja, Peter Mkwavila, Ibrahim Joseph na Renatha Msungu (DODOMA), Idda Mushi (Morogoro) na Julieth Mkireri (KIBAHA)***

## JPM atoa neno mchujo wagombea wa CCM

**Na Enock Charles**

RAIS John Magufuli amekagua maandalizi ya kumbi za mikutano na vikao vya chama vinavyotarajiwa kufanyika hivi karibuni katika jengo la Ofisi za Makao Makuu ya CCM (White House), Jijini Dodoma.

Katika taarifa iliyotolewa na Katibu wa Itikadi na Uenezi wa (CCM, Hunphrey Polepole, imeeleza kuwa Rais Magufuli akiwa ameongozana na Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Philip Mangula na Katibu Mkuu, Bashiru Ally, walikagua kumbi za Kituo cha Mikutano Dodoma ambako utafanyika Mkutano Mkuu wa CCM mwaka huu.

"Rais Magufuli amewapongeza wajumbe wa Sekretarieti ya CCM na wasimamizi wa ukarabati uliofanyika katika majengo hayo ya CCM ambayo yanatarajiwa kuwa tayari ifikapo Juni 20, mwaka huu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Magufuli alisisitiza kuwa pamoja na kufanyika kwa mchakato wa uchaguzi ndani ya chama, Uchaguzi Mkuu lazima utakuwapo na hivyo amewataka wanachama wote wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kujitathmini na kujiridhisha kama wanatosha kugombea nafasi wanazozoomba.

Ameonya kuwa kuelekea katika mchakato huo wanachama hawana budi kuweka mbele maslahi ya chama badala ya maslahi yao binafsi na pia kutofanya vitendo vya kuwagombanisha na fujo ambavyo vitakiumiza chama.

## HABARI KITAIFA

# Wateja kupata gawio la bil. 1/- Halopesa

**Na Beatrice Philemon**

KWA mara ya kwanza Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Halotel Tanzania italipa gawio lenye thamani ya shilingi bilioni moja kwa wateja wake wa Halopesa zaidi ya milioni 1.9 nchini kupitia huduma zake za kifedha za HaloPesa kuanzia mwezi huu wa Juni.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha HaloPesa, Magesa Wandwi, alisema kuwa gawio hilo litalipwa kwa wateja binafsi, mawakala wa kusambaza huduma za HaloPesa na washirika wake ambao wanatumia huduma za HaloPesa.

"Wateja wa HaloPesa watapata gawio hili linalotokana na faida iliyozalishwa kutoka katika akaunti za HaloPesa Trust, zilizoko katika benki mbalimbali nchini kati ya Oktoba 2016 na Desemba 2018," alisema.

Alisema faida hiyo ni haki ya wateja na HaloPesa wanashauku kuwalipa wateja wao gawio hilo kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali toka Benki Kuu ya Tanzania.

"Gawio hili ni la kwanza kwa wateja wetu na litatolewa ndani ya mwezi mmoja toka sasa, kiasi cha gawio ambacho mteja wa HaloPesa atakipata anaweza kutumia atakavyo ikiwa ni pamoja na kutoa au kufanya miamala mbalimbali," alisema.

Alisema Halotel inaendelea kutoa huduma bora zenye gharama nafuu nchi nzima na kuwaomba wateja waendelee kutumia huduma za Halopesa,

Pia, wamewakaribisha wateja wapya kutumia huduma za HaloPesa zenye huduma nafuu na pia kuwashukuru wadau wanaondelea kutumia huduma zao za HaloPesa.

"Tunaishukuru Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kutusimamia vizuri kwa sababu hizi ni pesa za wateja tunatimiza wajibu wetu wa kisheria na kanuni ili wateja wetu wanufaike," alisema.

# Tuico kuendelea kulinda wafanyakazi

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (Tuico), kimesema kitaendelea kulinda na kutetea maslahi ya wafanyakazi kutoka kwa waajiri wao wakiwamo wanaokiuka makubaliano ya kazi kwa kisingizio cha janga la corona na baadhi huwasimamisha kazi wafanyakazi bila makubaliano na kuzua migogoro kama ilivyojitokeza kwa kiwanda cha kutengeneza nguo cha mazava.

Mwenyekiti wa Tuico Taifa, Paul Sangeze, alisema hayo mjini hapa, alipokutana na wajumbe wa baraza la chama hicho, na kuwaasa waajiri kuzingatia makubalino na kusisitiza kutokuwa tayari kuona maslahi ya wafanyakazi yanakandamizwa.

Alitoa mfano walivyoweza kuhakikisha haki inapatikana kwenye mgogoro ulioibuka karibuni mjini Morogoro baina ya wafanyakazi wa kiwanda cha mazava na uongozi wa kiwanda hicho na kushukuru Ofisi ya Kamishna ya Kazi Tume ya Usuluhishi na Uamuzi CMA, Mkoa wa Morogoro, Ofisi ya Mkuu wa mkoa na mamlaka zingine kwa kushirikiana nao kufanikisha kutatua mgogoro huo mkubwa ulioibuka baada ya wafanyakazi kusimamishwa kazi kwa muda wa miezi mitatu kwa madai ya kusababishwa na athari za corona.

Sangeze alisema katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2019, Tuico imeendelea kutekeleza mpango mkakati wa chama hicho ikiwa ni pamoja kutatua migogoro baina ya wafanyakazi na waajiri, kuhamasisha wafanyakazi kulipa michango, kutoa mafunzo, kufanyaziara kwenye maeneo ya kazi na kudumisha uhusiano baina ya wafanyakazi na waajiri maeneo ya kazi.

Aliwataka viongozi, wafanyakazi na wanachama wa chama hicho kuendelea kuwa na umoja, mshikamano katika kutekeleza majukumu yao ili kuendelea kuwa chama cha mfano kwa wakati wote.

Rais wa Tucta, Tumain Peter Nyamhokya, alipongeza hatua ya Rais kujali wafanyakazi kwa kuendelea kuwalipa mishahara bila kufanya kazi wakati huu wa janga la corona.

Vile vile, aliwashauri wanachama wa Tuico kuwa makini kwenye uchaguzi wa chama hicho kwa kuchagua viongozi makini wanaoweza kukifikisha mbali chama hicho na uchaguzi ukiisha wavunje makundi ili kuwa wamoja kukijenga chama hicho.




Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, mkoani Mwanza, Ester Chaula (kulia) na Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Focus Majumbi (wa pili kulia), wakipokea msaada wa vitanda, magodoro, vifaa vya kuzimia moto, maboya ya kujiokoa kwenye maji, vyenye thamani ya Sh. milioni 95, kutoka kwa Meneja Mauzo Mwandamizi wa Vodacom Kanda ya Ziwa, Victoria Chale (kushoto) na Meneja Miradi wa Taasisi ya Sukos Kova Foundation, Rahma Kova, vilivyotolewa na Vodacom Tanzania Foundation, wilayani humo jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Chadema yaeleza sababu kukwama barua ya Msajili

**Na Mwandishi wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimesema kuwa kinashindwa kufanyia kazi barua ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini kutokana na zuio la mikusanyiko lililopo kwa sasa.

Wiki iliyopita Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Fransis Mutungi, alisema ameshaviandikia barua vyama vyote nchini kuhakikisha vinapeleka ratiba zao za masuala mbalimbali yanayoendelea ambayo kwa mujibu wa sheria anapaswa kuyajua, kueleka uchaguzi mkuu.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Mawasiliano na Itifaki, John Mrema, alisema barua ya Msajili imekuja wakati ambao serikali haijaondoa zuio la mikusanyiko.

"Kutokana na hali hiyo, tunashindwa kuweka ratiba ya vikao kwani hatuna uhakika juu ya zuio litaisha lini ili tuweze kuitisha vikao husika," alisema.

Juzi, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Magdalena Sakaya, alisema walijibu barua ya Msajili na kumuuliza suala la zuio la mikusanyiko kutokana na janga la corona, lakini hadi sasa kuna ukimya.

Sakaya ambaye pia ni Mbunge wa Kaliua, alisema kumekuwa na sitofahamu ndani ya chama hicho kwa kuwa kilipaswa kuanza kura za maoni jana na kumaliza mwisho wa mwezi huu, lakini wameshindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwapo kwa taarifa kuhusu mikusanyiko.

Kuhusu zuio la mikutano, Mrema alisema limewaathiri katika kukutana na wananchi na kuweleza Sera zao na upungufu wa chama tawala na kama wangeingia madarakani wangefanya nini cha utofauti.

"Hii ni fursa ambayo tumeikosa, wananchi wamekosa fursa ya kuwasikiliza viongozi wao na hivyo wamekuwa wakisikia ya upande mmoja wa walioko madarakani," alisema:

"Hali hii imewasababishia kiu na shauku ya kusikiliza sauti mbadala."

TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
TACOBA
"Our Bank for Our Development"

**KUAHIRISHWA KWA MKUTANO MKUU (WA SITA) WA MWAKA WA BENKI YA WANANCHI TANDAHIMBA - 2020**

Tunasikitika kuwaarifu wanahisa wetu kuwa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliokuwa ufanyike mnamo tarehe 20 June, 2020 kwenye Uwanja wa Majaliwa, Tandahimba Mjini; umeahirishwa.

TACOBA - Tukiwa Benki makini na inayojali; tunaungana na Serikali yetu kuepuka kuenea kwa virusi vya corona kwa kutekeleza agizo la kuepuka MIKUSANYIKO. Nyakati za changamoto kama hizi, usalama wa wanahisa, wateja, wafanyakazi na jamii yetu ni muhimu kuliko vyote.

Wanahisa, wateja na wananchi watajulishwa kwa wakati muafaka kuhusu maamuzi mengine yoyote yahusuyo mkutano huo.

Ukiwa na swali lolote, tafadhali wasiliana na Uongozi wa Benki kupitia +255 23 241 0093 au barua pepe: info@tacobabank.co.tz

John Baptist Rugambo
Katibu wa Benki
28/05/2020

Huduma BORA za Benki yetu zinaendelea kama kawaida
TACOBA – Benki YETU kwa Maendeleo YETU

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waliorejea shule, vyuoni wajihadhari corona bado ipo

**JANA** wanafunzi wa vyuo na wa kidato cha sita walirejea vyuoni na shuleni, baada ya serikali kuruhusu kutokana na kupungua kwa maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Serikali kupitia Waziri Mkuu, Kassim Mjaliwa, Machi 17, mwaka huu ilitangaza hatua mbalimbali za kukabiliana na maambukizo ya ugonjwa huo, ikiwamo kuzifunga shule na vyuo, kwa lengo la kuepisha misongamano hadi itakapotangazwa tena, baada ya kasi ya maambukizo kupungua.

Hata hivyo, takribani wiki mbili zilizopita, Rais John Magufuli alitangaza kufunguliwa kwa vyuo na kidato cha sita Juni Mosi (jana), ili wanafunzi wa kidato hicho wanaokabiliwa na mitihani ya taifa kujiandaa.

Rais Magufuli alifanya uamuzi huo ikiwamo kuruhusu kurejea kwa michezo hususan Ligi Kuu, FA Cup, Ligi Daraja la Kwanza na Daraja la Pili, huku akifanya uchambuzi wa takwimu mbalimbali katika hospitali nchini zilizokuwa zikionyesha kasi ya kupungua kwa wagonjwa.

Wanafunzi hao kukaa muda mrefu nyumbani takribani miezi mitatu kutakuwa kumeathiri kwa kiasi fulani programu za masoko kwa wanafunzi, walimu na wahadhiri.

Hata hivyo, tunaamini kuwa menejimenti za vyuo na shule zitabuni na kutekeleza mipango na mikakati mizuri kuhakikisha kwamba programu za masoko zilizopangwa kufundishwa zinakamilishwa bila kusababisha athari zozote.

Tunawashauri wanafunzi na wanavyuo kutambua kuwa wana kazi ya ziada ya kufidia viporo vya masomo. Jambo la kufanya ni kusoma kwa bidii na kufuata maelekezo yanayotolewa na viongozi wa taasisi zao.

Kikubwa ambacho tunashauri kwa taasisi hizo na wanafunzi ni kutambua kuwa bado ugonjwa wa corona upo, hivyo kuchukua tahadhari zote muhimu ambazo zinaendelea kutolewa na wataalamu wa afya.

Kwa kuwakumbusha baadhi ni kunawa mara kwa mara kwa kutumia maji tiririka na sabuni, kuvaa barakoa na kutumia vitakasa mikono (sanitizer). Tahadhari nyingine ni kukaa umbali wa angalau mita moja, kuepukana na misongamano, kuepuka kushikana mikono na kubusiana.

Uongozi wa vyuo na shule umeshapewa maelekezo na serikali kupitia mwongozi uliotolewa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, hivyo tunatarajia kuona tahadhari zote zikiwekwa kwa kipindi chote cha tishio la maambukizo.

Tunatarajia kuona taasisi hizo ziliweka ndoo zenye maji tiririka, sabuni, vikatasa mikono vikiwekwa katika milango ya kuingilia na hata ndani ya ofisi, mabweni, vyooni na maeneo mengine.


Vile vile, itakuwa vizuri kama taasisi hizo zitakuwa zikiwapima joto la mwili wanafunzi, wafanyakazi na watu wengine wanaoingia ndani.

Upo umuhimu pia wa wataalamu wa afya kwenda katika taasisi hizo kufuatilia kama maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya yanatekelezwa, na pale itakapobainika vinginevyo, hatua kali za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Kadhalika, tunaona kuwa kuna umuhimu wa wataalamu wa afya kuweka utaratibu wa kwenda kutoa elimu na msisitizo kwa wanafunzi kuendelea kuchukua tahadhari. Ni matarajio yetu kuwa kila mmoja aliwajibuka na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya, ugonjwa huo tutaushinda, na tutavuka salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kampeni hizi zisambae zaidi kunusuru mabinti

Na Sabato Kasika

**KISWAHILI** kina msemo 'ukimsomesha mtoto wa kike, utakuwa umeelimisha taifa zima' na ufafanuzi zaidi unafuata kuwa ukiwekeza elimu kwa mtoto wa kike kuna mafanikio makubwa na manufaa zaidi.

Hizo zote ni njia zinazohamasishwa na wadau wa elimu kwa lengo la kubadilika na kumsomesha watoto bila ubaguzi, kwa vile wote wana haki ya kupata elimu na kujileta maendeleo.

Wakati kukiwa na kampeni hizo, bado wapo baadhi wasiotambua umuhimu huo wa kumsomesha mtoto wa kike, badala yake wanawaingiza kwenye vitendo ambavyo vinawakwamisha kielimu.

Kwa mfano tangu shule zifungwe Machi mwaka huu, kupunguza maambukizo ya virusi vya corona, baadhi ya wanafunzi wa kike wamekumbana na changamoto zinazoweza kuwakwamisha kielimu.

Wanafunzi hao ni wa wilayani Serengeti mkoani Mara, ambao wamekutana na sintofahamu hiyo ambayo ya kuandaliwa kwa ajili ya kukeketwa, badala ya kuachwa wajisomee wakati wakisubiri shule zifunguliwe.

Katika wilaya hiyo vitendo vya ukeketaji vinadaiwa kufanyika huku zikiwa zimefungwa na kuwafanya wakose amani, hali iliyosababisha wadau wa elimu kuingilia kati na kuanzisha kampeni za kuwanusuru.

Lengo la kuanzisha kwa kampeni hizo si kuwaepusha dhidi ya ukatili huo, bali ni kutaka waachwe wawe na muda wa kujisomea ili shule zitakapofunguliwa wawe na kitu walichojifunza wakiwa nyumbani.

Hope for Girls and Woman Tanzania ni moja ya wadau wa elimu ambao kwa kushirikiana na vyombo vya dola, wanafanya kampeni za kuwanusuru wanafunzi dhidi ya ukeketaji ambazo zilianza tangu Aprili mosi mwaka huu.

Katika kampeni hizo, tayari wamepatikana wanafunzi 47, huku baadhi yao wakiwa tayari wamekeketwa, na pia zinaambatana na elimu kwa jamii ili iachane na mila hizo, ambazo zimepitwa na wakati.

Hivyo ndivyo, anavyosema Mkurugenzi Mtendaji wa Hope, Rhobi Samwelly na kufafanuwa kwamba, licha ya juhudi mbalimbali za kukomesha vitendo vya ukatili huo, bado vitendo bvya ukeketaji vipo ndani ya jamii.

Kwa maelezo hayo ya Rhobi ni wazi kwamba bado kuna safari ndefu ya kuibadili jamii ya huko, ili iachane na mila potofu zinazokandamiza mtoto wa kike na kusababisha akose elimu.

Hii inatokana na kile kinachoelezwa na baadhi ya wenyeji wa huko kwamba msichana akishakeketwa huwa anaandaliwa kwa ajili ya kuolewa, hivyo kama ni mwanafunzi, anaweza kukatishwa masomo na kuingiza kwenye ndoa.

Hivyo ni vyema kampeni hizo za kupambana na ukeketaji zikasambaa maeneo yote ya mkoa wa Mara ambayo yanadumisha mila hizo kuwanusuru wanafunzi ili waendelee kujisomea wakati wakisubiri shule zifunguliwe.

Serikali na shule zinajitahidi kutoa elimu kwa wanafunzi wakiwa nyumbani, lakini inasikitisha kusikia wapo baadhi ya wazazi ambao badala ya kuwaacha watoto wajisomee, wanawapeleka kwa ngariba wakeketwe.

Ingependeza kama mzazi au mlezi angemtafutia mtoto wake mwalimu wa kumfundisha masomo mbalimbali kuliko kumtafutia ngariba ambaye ni hatari kwa maisha na hata kwa maendeleo yake ya elimu.

Serikali ilishaweka wazi kwamba wanafunzi wameruhusiwa nyumbani ili kuepushwa na maambukizo ya virusi vya corona, lakini ikiwasisitizia wazazi kutowaruhusu kuzurura ovyo.

Inasisitiza hivyo na kuwataka wahakikishe wanabaki nyumbani wakijisomea, na ndiyo maana imeanzisha vipindi vya masomo kupitia vyombo vya habari ikiwamo televisheni ili wanafunzi wasome.

Si hapo tu bali shule nazo zimekuwa zikisambaza masomo kwa wanafunzi, lengo ni kutaka wanafunzi wasiwe na muda wa kukaa bila kujisomea ili mwisho likizo ya corona wawe kama hawakuwa likizo.

Kwa hiyo wanaokwenda kinyume na maelekezo hayo na kuingiza watoto wao katika hatari ya kukeketwa, ni vyema wakafuatiliwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ili kukomesha mila hizo.

Ufuatiliaji wa vitendo vya ukeketaji lisiwe jukumu la serikali na baadhi ya asasi za kiraia tu, bali raia wote kila mmoja kwa nafasi yake ana wajibu wa kufanikisha kampeni kukomesha ukeketaji Serengeti na kwingineko.

HABARI KITAIFA

# Mafunzo yatolewa kuondoa hofu corona

**Anthony Gervas,** MWANZA

SERIKALI imeiasa jamii kushirikiana na wataalamu wa huduma za kijamii ili kutoa elimu ya kisaikolojia kwa lengo la kukabiliana na maambukizo ya virusi vya ugonjwa wa corona (Covid 19).

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi Msaidizi wa huduma za ustawi wa jamii katika Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Rasheed Maftah, jijini Mwanza, kwenye mafunzo ya kutoa msaada wa kisaikolojia kwa jamii (PSS).

"Mafunzo hayo yameshirikisha washiriki 50 kutoka wilaya za Nyamagana na Ilemela na mashirika mbalimbali yanayojishughulisha na utoaji wa shughuli za ustawi wa jamii ili kuwajengea uwezo wawezeshaji wa huduma za kisaikolojia kwa jamii," alisema Maftah.

Maftah alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa kazi iliyoanzishwa na ofisi ya Rais John Magufuli ya kupambana na hofu ya ugonjwa wa virusi hivyo nchini.

Alisema mafunzo haya ni mwendelezo mafunzo yaliyotangulia kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Plan International na wadau mbalimbali walioandaa mafunzo hayo yenye lengo la kuwajengea uwezo wataalamu hao ili waende kutoa huduma kwenye vituo vinavyotoa tiba.

Alisema kuwa mafunzo yameshatolewa kwa mikoa 10 kuanzia Dar es Saalam, Kilimanjaro, Arusha, Songwe, Mbeya, Kigoma, Mwanza, lakini lengo ni kuifikia mikoa yote Tanzania ili kuwaondoa hofu wananchi juu ya ugonjwa huo wa corona.

**Mafunzo hayo yameshirikisha washiriki 50 kutoka wilaya za Nyamagana na Ilemela na mashirika mbalimbali yanayojishughulisha na utoaji wa shughuli za ustawi wa jamii ili kuwajengea uwezo wawezeshaji wa huduma za kisaikolojia kwa jamii**

# Benki za TPB, Posta zaunganishwa rasmi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeunganisha rasmi Benki ya Uwekezaji Tanzania(TIB Corporate Limited) na Benki ya Posta Tanzania (TPB blank Plc) ili kuwa na benki mahsusi ya biashara.

Katika muunganiko huo, TPB imechukua mali na madeni TIB na kwa sasa itakuwa inamiliki amana za Sh. bilioni 700 na mali za Sh. trilioni moja.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Msajili wa Hazina, Athumani Mbuttuka, alisema uamuzi huo ni utekelezaji wa tamko la Rais la kutaka kuwa na benki moja yenye kutoa huduma nzuri na za kiufasaha.

"Kuanzia leo Juni mosi 2020, katika hatua ya awali, Benki ya TPB itachukua mali na madeni ya TIB," alisema.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kuifanya benki kuwa imara, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji.

Mbuttuka alisema muunganiko huo ni hatua mojawapo inayochukua zenye lengo la kuboresha utendaji wa mashirika na taasisi za umma na hautaathiri huduma za kibenki.

"Tunawahakikishia hakutakuwa na shida yoyote katika utendaji hivyo wateja wawe na amani hakuna kitakachoharibika," alisema Mbuttuka.

Alisema muunganiko huo unalenga kuleta mageuzi makubwa ya kiutendaji kimfumo, kimuundo na kitaswira ili benki hiyo iweze kuhimili ushindani wa kibiashara kwenye sekta ya fedha.

"Serikali inapenda kuhakikisha umma kuwa itaendelea kuhakikisha utendaji wa benki zake unaimarika," alisema.

Alisema wateja wote wa benki za TPB wataendelea kupata huduma kwenye matawi yao kama kawaida.

Alieleza kuwa hivi sasa wanaamini Benki ya TPB itakuwa ikifanya kazi kiufasaha tofauti na ilivyokuwa awali.

Akizungumzia suala la wafanyakazi, alisema hakuna atakayefukuzwa kazi kwa kuwa si mara ya kwanza kwa benki kuungana.



Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Liwale, mkoani Lindi, wakishiriki kutengeneza barabara ili kurahisisha shughuli za usafirishaji wa vifaa vya ujenzi wa hospitali mpya ya wilaya hiyo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Waitwa kujenga viwanda vifaa vya gesi

**Na Said Hamdani, LINDI**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewaomba wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kwenda mkoani Lindi, kujenga viwanda vitakavyohusika na utengenezaji wa vifaa.

Vifaa hivyo ni pamoja na vya Luku zitakazotumika katika usambazaji gesi asilia kwa wateja wa nishati ya kupikia majumbani.

Dk. Kalemani alitoa ombi hilo, wakati wa hafla ya uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi ya kupikia majumbani, uliofanyika Mtaa na Kata ya Mnazi-Mmoja Manispaa ya Lindi.

Akizungumza na wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi huo, Waziri Kalemani alisema kutokana na mikoa ya Lindi na Mtwara ndiko ilikogunduliwa rasilimali hiyo, upo umuhimu mkubwa wa kujenga kiwanda kitakachohusika na utengenezaji wa nyaya na Luku zitakazotumika kupitishia gesi asilia itakazofungwa majumbani.

Waziri huyo alisema kujengwa kiwanda katika mkoa wa Lindi kutakuwa na manufaa zaidi ikiwa ni pamoja ongezeko la uchumi wa Taifa na kuipunguzia serikali mzigo wa kuagiza vifaa husika nje ya nchi, na kuongezeka kwa ajira kwa Watanzania wengi.

"Kama gesi asilia imepatikana huku Lindi na Mtwara, hakuna sababu ya kutokuwapo kwa kiwanda cha kutengeneza Luku au nyaya za kupitisha gesi," alisema Waziri Kalemani.

Alisema mradi huo wa matumizi ya gesi majumbani utaleta unafuu katika matumizi ya kila siku katika kupikia na shughuli nyingine, hali itakayochangia wananchi kuachana na matumizi ya kuni, mkaa na kupunguza gharama kwa kununua nishati hiyo.

Waziri Kalemani alisema mradi utakapokamilika na kuanza kazi, kilo moja ya gesi itaweza kutumiwa kwa zaidi ya siku tatu kwa gharama ya Sh. 1,000 tu badala ya kuni au mkaa, huku akiwasisitiza wananchi wa Lindi na vitongoji vyake kuchangamkia fursa hiyo muhimu.

Alisema serikali imebeba gharama zote za usambazaji na uunganishaji wa huduma hiyo majumbani, huku akiwataka wataalamu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) na kampuni ya Gasco kutowatoza fedha kama gharama za kuwapelekea wateja gesi hiyo kwani tayari mzigo huo umeshabebwa na serikali.

Mwanzoni akitoa taarifa wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio, alisema mradi utakapokamilika utawanufaisha wananchi waishio kata tatu za Mnazi-Mmoja, Mingoyo na Kiwalala, huku mitaa itakayopelekewa kwa awamu ya kwanza ni 23.




Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (wa nne kushoto), akikabidhi mkopo wa Sh. millioni 200 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), kwa Chama cha Ushirika wa Wavuvi Bukasiga kilichopo wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**.

# Wana-CCM mbaroni kwa madai rushwa ya uchaguzi

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imewakamata wanachama 6 wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa madai ya kujihusisha na rushwa katika uchaguzi wa ndani wa chama hicho.

Katika taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kinondoni, Pilly Mwakasege, imeeleza kuwa watuhumiwa hao walikamatwa na maofisa wa Takukuru wakiwa wakiwa katika harakati za kupokea bahasha zenye fedha kutoka kwa mtia nia mmoja kutoka ndani ya chama hicho.

"Kupitia operesheni hii, jumla ya bahasha 9 zilikamatwa na kila bahasha ilikuwa na Sh. 50,000, pia ndani ya mkoba wa mtia nia zilikutwa Sh. 240,000 ambazo zilikuwa kwenye mchakato wa kugawiwa kwa wajumbe hao na hivyo kufanya jumla ya Sh. 690, 000," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Watuhumiwa hao ni Lida Lugano Mwakatuma ambaye ni mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM tawi la Azimio, Aisha Muki Katibu kata CCM Kata ya Mbezi, Subira Emmanuel -Katibu UWT Kata ya Mbezi , Charles Haule Denga ambaye ni mjumbe wa kamati ya siasa kata ya Mbezi na Angela Paulo, ambaye ni mjumbe wa kamati ya siasa Kata ya Mbezi.

Katika taarifa hiyo imeelezwa kuwa, mtuhumiwa Lida Lugano Mwakatuma, mkazi wa Goba, jijini Dar es Salaam ndiye aliyeitisha kikao cha siri na wajumbe wengine alitoroka na kuacha vitu vyake ikiwamo kadi ya mpigakura na gari lake.

# DC Tunduru amtumbua ofisa biashara

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, amemwondoa Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, Anderw Macha, kwa tuhuma za kuwanyanyasa wafanyabiashara wa halmashauri hiyo.

Inadaiwa ofisa huyo pia alikuwa anawanyanyasa wafanyabiashara ya ufuta kwa lengo la kutaka kupewa rushwa.

Katika taarifa hiyo Mtatiro alisema ofisa huyo amekuwa akitumia utaratibu wa kukwamisha uandikaji wa vibali kama sehemu ya shinikizo hilo.

Alisema awali alilazimika kumwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kubomoa droo ya meza yake na kuchukua vitabu na kumpatia mtu mwingine ili awaandikie vibali na kuwafanya wafanyabiashara hao waondoe mizigo yao.

Aidha, katika tukio hilo, Mtatiro alimuweka ndani kwa saa 24 na kumwagiza mkurugenzi kumrudisha kwenye ajira ya ualimu alikotokea kabla ya kuwa ofisa biashara.

Alisema mara ya kwanza ofisa huyo alitafutwa kwa ajili ya shughuli hiyo akasingizia kuwa alikuwa shambani na mara ya pili ilionyesha kuwa alikuwa ameweka msimamo wa kutofanya shughuli hiyo kwa vile ilikuwa siku za mwisho wa wiki.

"Hatuwezi kuendelea kupotezea watu muda wakati maelekezo ya serikali yanatutaka kuwavutia wawekezaji," alisisitiza, Mtatiro.

Mtatiro pia alionekana kukerwa na taarifa za kuwapo kwa unyaufu katika ufuta ulionunuliwa na wafanyabiashara unaofanywa na maofisa wa bodi inayosimamia maghala.

Alisema hizo ni mbinu za kuwaibia wanunuzi stahiki zao na wao kujinufaisha, jambo ambalo alisema halikubaliki.

# Mch. anayedaiwa kumpa mimba mwanafunzi kusimama kortini leo

**Na Salome Kitomari**

MCHUNGAJI wa kanisa la Mlango wa Ukombozi Gairo, mkoani Morogoro, Joseph Gervas (28), atafikishwa mahakamani leo kwa ajili ya kujibu tuhuma za kumbaka na kumpa mimba mwanafunzi wa kidato cha tatu mwenye umri wa miaka 17(Jina limehifadhiwa).

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Kamanda wa Polisi mkoa wa Morogoro, Willibroad Mutafungwa, alisema tukio hilo lilitokea Mei 27, mwaka huu katika kijiji cha Rubeho kata ya Kisitwi,Tarafa ya Gairo wilayani Gairo.

"Tumeshakamilisha upelelezi wetu na mtuhumiwa anafikishwa mahakamani kesho (leo) kwa kosa la ubakaji na kumpa mimba mwanafunzi huyo," alisema.

Kuhusu kuwa na uhusiano na mama wa binti huyo, alisema mama huyo amehojiwa na polisi lakini hakukiri hilo na kwamba mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani kwa kosa la ubakaji.

Wiki iliyopita, Kamanda Mutafungwa aliieleza Nipashe kuwa mchungaji huyo alianzisha kituo cha maombi nyumbani kwake na kwamba mwanafunzi huyo alikuwa na tatizo na uoni hafifu, wazazi walishindwa kumnunulia miwani na kuamua kumpeleka kwenye maombi.

Kamanda huyo alisema mahudhurio ya binti huyo shuleni hayakuwa ya kuridhisha na wanaendela kufuatilia kwa kina.

"Akiwa kwenye kituo hicho Mchungaji akaanza kumuingilia toka mwaka jana wakati mke wa mchungaji akisafiri au kwenda shamba, huku akimwaminisha ndiyo namna ya kupona tatizo lake," alisema.

Kamanda Mutafungwa alisema binti huyo alipokwenda kwa wazazi wake waliona ana dalili za ujauzito na walipompima walibaini ana mimba, alivyohojiwa alikiri kuwa na uhusiano wa kingono na Mchungaji huyo.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Gairo, , Siriel Mchemba, alisema katika kituo hicho kulikuwa na mabinti wengine wawili.

Alisema wakiwa kwenye mkutano wa hadhara wanawake wengine waliibuka na kueleza kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji.

# Baba mbaroni madai kuua mwanawe kwa mapanga

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

POLISI wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wanamshikilia mkazi wa Kitongoji cha Ngalinje katika kijiji cha Liwangula Kata ya Mindu, Amanzi Amanzi (37) kwa tuhuma za kumuua mtoto wake kwa kumkatakata kwa mapanga.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa kufutia ushirikiano mkubwa uliotolewa na wakazi wa kitongoji hicho.

Alisema mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya kukamilika kwa taratibu za awali za mahojiano.


Mwenyekiti wa Kitongoji cha Ngalinje Kijiji cha Liwangula, Husein Hamisi Ngauje, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Mei 26, mwaka huu baada ya mtuhumiwa huyo kumwagiza mkewe akamchulie maji ya kunywa.

Alisema kilichomshangaza aliporudi alimkuta mtuhumiwa ambaye alimuacha akiwa amemlaza kwenye mkeka uliokuwa umetandikwa uwani akiwa anamcharanga kwa mapanga marehemu Nasri Amanzi mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu.

Alisema baada ya tukio hilo mtuhumiwa huyo alitoka nje na kutokomea kusikojulikana, hali ambayo ilimfanya mama wa mtoto huyo, Amina Bakari, kupiga kelele za kuomba msaada na kuanza taratibu za kutaka mtoto wake apelekwe hospitali.

Alisema wakiwa katika harakati hizo mtoto alifariki dunia, hali ambayo iliwafanya watoe taarifa polisi na baadaye kuanza kumtafuta mtuhumiwa.

Alisema baadaye Polisi walienda katika eneo la tukio na kuwaruhusu kufanya maziko.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo (wa pili kushoto), na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mhandisi Cyprian Luhemeja (wa pili kulia), wakionyesha mkataba wa makabidhiano ya Bohari Kuu ya Maji pamoja na miradi ya maji iliyokuwa inaendeshwa na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam kwa Dawasa, jijini humo mwishoni mwa wiki. Wanaoshuhudia ni Naibu Katibu Mkuu wizara hiyo, Mhandisi Antony Sanga na Mkurugenzi wa Wizara ya Maji, Nadhifa Kemikimba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapewa mil. 200/- ujenzi kiwanda

**Na Neema Emmanel, UKEREWE**

KATIKA kuelekea kwenye uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ifikapo 2025, Chama cha Ushirika wa Wavuvi Bukasiga kilichopo wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, kimekabidhiwa mkopo wa Sh. milioni 200 kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha barafu na kujenga mtambo wa kukaushia dagaa ili kuongeza thamani ya samaki na mazao yake.

Akizungumza wakati akikabidhi hundi hiyo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema ili kufikia adhima hiyo, lazima wavuvi hao wachape kazi kwa nguvu kwa sababu hakuna njia ya mkato ya kufikia maendeleo.

Alisema serikali imeweka mikakati mizuri na kuthubutu kuhakikisha wavuvi wanaanza kuaminika na kukopeshwa kupitia TADB na Rais Magufuli ameweka mazingira ya kufanya wavuvi waweze kuaminika na taasisi za kifedha na kupewa mikopo ili kujiimarisha katika shughuli zao.

"Hii benki tangu ianze ina miaka mitano, na katika miaka mitano ya Rais John Magufuli imewakopesha Watanzania katika nyanja za kilimo, mifugo na uvuvi zaidi ya Sh. bilioni 170 na tangu uhai wa taifa hili wavuvi wameanza kuaminika na kukopeshwa pesa, pia samaki siyo zao la msimu ni la mwaka mzima, hivyo wakati ndio huu wa kutimiza lengo la Rais la kuwa na viwanda vidogo vidogo vitakavyoleta tija na maendeleo kwa wananchi na kukuza uchumi wa nchi," alieleza Ulega.

Aliwataka kuwa wazalendo, waadilifu katika kusimamia vyema fedha walizopata, huku akiitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) wilayani humo kuwashauri wanachama hao mapema kuliko kusubiri mpaka waharibikiwe na kutoa onyo kwa watendaji kutotegemea posho katika kutimiza majukumu yao bali wafanye kazi pasipo kuweka vikwazo.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema uvuvi ni eneo muhimu katika Ziwa Victoria kwani samaki wanapatikana kwa wingi, hivyo kinachohitajika ni kufanya uvuvi wa kisasa ili kubadilisha rasilimali kuwa fursa.

# RC atoa mwezi wa vitambulisho

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, ametoa mwezi mmoja kwa viongozi wa halmashauri zote kuhakikisha wamemaliza kugawa vitambulisho vya wajasiriamali, ambavyo vimetolewa hivi karibuni.

Alisema hakuna sababu ya kuchukua muda mrefu katika ugawaji wa vitambulisho hivyo kwa sababu wameshapata uzoefu kutokana na vya mwaka jana.

Mwanri alitoa agizo hilo, mjini Igunga wakati wa mkutano wake na watendaji wa kata na vijiji kuhusu umuhimu wa kutekeleza zoezi hilo.

Alisema utendaji wa mtendaji yoyote utapimwa pamoja na majukumu mengine ni pamoja na jinsi atakavyofanikisha zoezi la kuwezesha wajasiriamali wadogo na watoa huduma kuchukua vitambulisho.

Mwanri aliongeza kuwa kila watakapokuwa wakiuza kitambulisho wahakikishe fedha wanazipeleka benki au wanalipa kwa wakala wa benki kwa kutumia 'Control namba'.

# Askofu akerwa kelele za muziki

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Tabora, Mhashamu Paul Ruzoka, amevitaka vyombo vinavyosimamia sheria za uendeshaji wa sehemu za starehe hasa kwenye baa kuhakikisha sauti za miziki inayopigwa hauleti kero kwa watu wengine.

Hali hiyo inatokana na kuzuka kwa tabia ya baadhi ya wamiliki wa baa jirani na Chuo cha Utumishi wa Umma (UHAZILI) kufungulia muziki kwa sauti ya juu usiku kuchwa na kusababisha wakazi walio jirani kushindwa kulala.

Askofu Mkuu Ruzoka alitoa kauli hiyo Jumapili wakati wa mahubiri na kuongeza:

"Katika maeneo hayo kuna watu wanahitaji utulivu ili waweze kusali, lakini wanashindwa kwa sababu miziki inafunguliwa inakera...kuna wagonjwa katika maeneo hayo wanahitaji utulivu, lakini miziki inayopigwa inawaongezea maumivu, kuna watu wanataka kupumzika baada ya majukumu, lakini hawapati haki yao kwa sababu ya kelele."

Alisema upo uwezekano watu wanaosimamia utekelezaji wa sheria ni wateja wa maeneo hayo, ndio maana wameshindwa kusimamia sheria za uendeshaji wa baa hizo ili kulinda za watu wengine.

Askofu Ruzoka aliongeza hata wanaokuwa katika maeneo hayo hawazingatii maelekezo ya wataalamu wa afya ya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 wa kukaa umbali walau mita moja na nusu

# Hapi ataka mapato kurejeshwa Mufindi

Na Francis Godwin, IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, imeitaka Halmashauri ya Mufindi kuhakikisha inaweka utaratibu wa kukusanya madeni yanayofikia shilingi 55,586,413.

Madeni hayo yametokana na wakusanyaji wa mapato katika vyanzo mbalimbali kama ilivyobainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2018/2019.

Agizo hilo lilitolewa jana na Hapi wakati wa kikao cha kupokea hoja za CAG kwa mwaka 2018/2019.

Alisema taarifa zilizopo ofisini kwako zinadai kuwa, hadi Aprili, 2020 halmashauri inayo madeni yanayofikia kiasi cha Sh. 232,918,374.22 ambazo ni fedha zilizokusanywa kwa kutumia POS na bado zipo mikononi mwa wakusanya mapato.

Alisema Katibu Tawala Mkoa alitoa maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa ambao walitakiwa kutekeleza ipasavyo kuhusu suala hilo, na halmashauri hiyo ihakikishe Sh. 232,918,374.22 zinazodaiwa kutoka kwa wakusanya mapato zinafuatiliwa, zinarejeshwa na kupelekwa benki kabla au ifikapo Juni 5, mwaka huu.

# Mradi mkubwa maji wanukia kukamilika

Na Anthony Gervas, MAGU

BENKI ya Maendeleo ya Ufaransa kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, zinatekeleza ujenzi mradi mkubwa wa majisafi na salama wilayani Magu mkoani Mwanza.

Halmashauri hiyo imeeleza kwamba mradi huo utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 14.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Elisha Hilal, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza mjini Magu na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi huo unaotarajiwa kukamilika mapema mwaka huu.

"Mradi huu wa majisafi na salama ya bomba umefadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ufaransa pamoja na Serikali ya Tanzania, na unaotarajiwa kuhudumia wakazi wa Magu mjini zaidi ya 4,000 na kata jirani za wilaya hiyo," alisema Hilal.

Hilal alisema mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2017 kwa lengo la kuondoa kero ya maji kwa wakazi wa mjini humo,iliyodumu miaka mingi, huku akisisitiza kuwa wananchi wanatakiwa kuutunza na kuuthamini utakapoanza.

Maji ya mradi huo yatasukumwa na mitambo kutoka Ziwa Victoria, ikiwa ndoto ya wakazi hao kupata maji bomba na kumaliza kero hiyo imetimia.

Aidha, alisema mradi huo utakuwa ni faida ya watu wengi na ambao wananchi wanatakiwa kuutunza na kuuthamini, hivyo watakaokamatwa wakiuhujumu watachukuliwa hatua za kisheria.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha Halopesa, Magesa Wandwi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, juu ya utoaji wa gawio kwa wateja wa Halopesa wakiwamo mawakala, wateja binafsi na washirika wake kuanzia mwezi huu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Mazao yatakayouzwa kwa stakabadhi ghalani yatajwa

Na Mwandishi Wetu

SERIKALI imetangaza rasmi mazao ya kuanzia yatakayouzwa kupitia mfumo maalumu wa uuzaji wa Mazao hayo ni korosho ambalo limekuwa na mafanikio makubwa kupitia mfumo huo. Mengine ni ufuta ambao utauzwa kwa mfumo huo katika baadhi ya maeneo nchini.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alitangaza uamuzi huo wa serikali wakati akizingumza ofisini kwake jijini Dodoma Jumamosi, huku akiyataja mazao mengine yaliyoingizwa katika mfumo huo kuwa ni pamoja na choroko, pamba, dengu na kahawa kwa baadhi ya maeneo.

Alisema mfumo huo tangu umeanza kutekelezwa umekuwa na faida kubwa hususani katika mikoa ya kusini kupitia zao la korosho, lakini umeleta changamoto kubwa katika maeneo ambayo misingi ya kuanzishwa kwa mfumo huo haijatimizwa.

Alisema ili mfumo wa stakabadhi ghalani uweze kufanya kazi kwa weledi na ufanisi mkubwa, ni lazima kuwa na vyama vya ushirika vya mazao vilivyoanzishwa na wananchi wenyewe katika eneo husika.

Kwa mujibu wa Hasunga, lengo la kuwa na vyama hivyo ni kufanya kazi ya kukusanya mazao na kuyapeleka kwenye ghala kuu ambalo limesajiliwa na kuwa na viwango vinavyotakiwa.

"Jambo jingine ni lazima kuwapo na mwendesha ghala mwenye leseni anayetambuliwa na Bodi ya Maghala na lazima elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ya namna ya kutumia mfumo huo na ushiriki wao katika kufuatilia minada itakavyokwenda," alisema.

Alisisitiza kuwa ili mfumo huo uweze kufanya kazi vizuri, wanunuzi lazima wawapo, na pia utangazwe na kuuzwa hadharani.

Kadhalika, kuwe na mzigo wa kutosha pamoja na ubora wa uhifadhi ili kuwavutia wanunuzi.

Alieleza kuwa sio mazao yote yanaweza kutumika katika mfumo wa stakabadhi ghalani ni baadhi ya mazao kulingana na uwezo wake wa kutunzwa na kukaa muda mrefu Akiwataka wafanyabiashara watakaonunua mazao hayo kwa mzigo unaozidi tani moja ni lazima Kodi za Halmashauri zilipwe kwa mujibu wa utaratibu wa kikanuni na kisheria.

Aliongeza kuwa moja ya majukumu ya wakuu wa mikoa na wilaya katika mfumo wa mazao ya stakabadhi ghalani ni kusimamia biashara kwa kuzingatia taratibu bila wananchi kudhulumiwa.

# Mahakama yashindwa kumsomea msimamizi mirathi ya Daudi Balali

Na Hellen Mwango

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeshindwa kumsomea msimamizi wa mirathi Elizabeth Balali (54), maelezo ya awali ya kesi ya mirathi ya marehemu Daudi Balali, baada ya mshtakiwa huyo kushindwa kufika mahakamani.

Kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali, lakini hakufika mahakamani wala mdhamini wake.

Mshtakiwa anakabiliwa na tuhuma za kujipatia Sh. milioni 25 kwa njia ya udanganyifu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Godfrey Isaya.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa kati ya Oktoba 19 na Desemba 21, 2017 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni 25 kutoka kwa Dk. Roderick Kisenge, kwa ulaghai.

Ilidaiwa kuwa alijipatia fedha hizo baada ya kujifanya anamuuzia eneo la mita za mraba 900 ambazo halijapimwa lililopo eneo la Boko Dovya, Kinondoni wakati akijua eneo hilo si lake.

Mshtakiwa alikana mashtaka hayo.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

Hakimu alisema mshtakiwa atakuwa nje kwa dhamana kwa kuwa na mdhamini mmoja atakayetia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni tisa.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 2, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Licha ya corona Makumbusho Kidijitali yang'ara D' Salaam**



Ukurasa 13

Misitu inavyotikisa maabara zinazosaka tiba ya corona



Ukurasa 12

**Kasa kutamia, ngadu mitini, ni maajabu hifadhi baharini**

ELIMU

**NA MICHAEL ENEZA**

# Kupeana nafasi wangapi watarudi kwa mwaka au watasomea wapi?

WAKATI wanafunzi wanarudi vyuoni na kidato cha sita, suala linaibuka kuhusu mbinu za kuhakikisha kuwa wanaendelea na masomo, huku tahadhari zikichukuliwa kuhusu kusambazwa virusi vya corona.

Kwa kukisia kwa karibu, matazamio ya wakuu wa idara tofauti serikalini na uongozi wenyewe ni kuwa hatari ya corona iendelee kupungua kwa kasi hii ya sasa, na shughuli zirudi kama kawaida.

Ikiwa hivyo, Tanzania na labda nchi kadhaa nyingine za Afrika, au labda kwa wingi wao, zitakuwa visiwa ambako janga la corona limepita pembeni, wakati dunia ikihangaika na maelfu ya vifo.

Hata hivyo matazamio hayo hayawezi kuwa msingi wa kusimamia sekta za uchumi kwa jumla na elimu kwa upande mwingine, ambayo ni sekta ya huduma za jamii kama ilivyo tiba.

Kukaa katika mfumo huo wa matazamio ni kuweka elimu rehani, ambako watu 10 wakipata corona katika kipindi kifupi, hatua za kwanza za kufunga mashule zinaanza upya, jambo ambalo haliwezekana.Unatakiwa mfumo wa kusimamia elimu kwa watoto na vijana wadogo, bila kuhatarisha afya zao na za familia pia.

Licha ya kuwa serikali ilitangaza kurudi shuleni kwa vijana wa kidato cha sita kwani wanaojiandaa kwa mitihani ya kitaifa, wakati inaangalia hali inavyokwenda kuhusu maambukizo ya corona kabla ya kufikia uamuzi kuhusu shule za msingi na sekondari, kuna kigezo kingine.



Wanafunzi wa vyuo vikuu kote nchini, wameanza masomo jana baada ya serikali kufunga taasisi hizo mwezi Machi kuepusha kuenea virusi vya corona. **PICHA: MTANDAO**

**KUHITAJI NAFASI**

Kurudi shuleni na vyuoni pia kumeambatana na hitaji la kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapeana nafasi wawapo darasani au katika mabweni.

Ndiyo maana inavyoelekea kuna ulazima wa mazingira ya uendeshaji wa sekta tofauti kijamii ubadilike, uendane na mahitaji ya janga la corona, ambako hadi sasa tunaweza kusema tumepona, ukilinganisha na kinachotokea maeneo mengi duniani, hata kwa majirani zetu. Ina maana kuwa licha ya kwamba sisi ni kisiwa cha kuibana corona kwa kiasi fulani, bado kuna tahadhari ya muda mrefu tunayotakiwa kuitilia maanani, ili tusije kujifunza kwa njia ngumu zaidi, endapo kutojali kutatoa mwanya kwa maambukizo kupanuka kwa kasi. Na bado katika mazingira hayo elimu ya chini iendelee.

Dhana ya kupeana nafasi ndiyo itakayobadili kimsingi jinsi elimu inavyosimamiwa, kwani hitaji la kwanza la kila mtoto kupata elimu limefikiwa kwa kiwango fulani, ila katika mazingira ya watoto kutumia nafasi ndogo ya darasa ukilinganisha na miongozo iliyofuatwa kwa miaka mingi hapo awali.

Tatizo lilikuwa ukifuata miongozo ya idadi ya wanafunzi na waalimu kwa darasa moja, ukubwa wake na vifaa, utaishia kuwa na shule chache zenye ubora, na watoto wengi kubaki nyumbani bila elimu, wakitegemea makuzi kwa utamaduni wa makabila yao. Serikali ikakataa hilo.

Janga la corona linaingia na 'rungu' la kupasua utulivu huo kwa kuhitajika kuwapa watoto na vijana wadogo wa sekondari elimu katika mazingira ambako hawajazani. Haitakuwa vyema kutumia shule zilizopo 'kwa nafasi' halafu wengine wabaki nyumbani, ila kubadili mfumo wa matumizi ya raslimali ili elimu iwe na kipaumbele cha pekee, ikiwa ni pamoja na kutumia maeneo ya wazi yaliyojengwa, ambayo yamepigwa na corona hayawezi kutumika kiuchumi kwa ufanisi.

Ni njia pia ya kuelekeza uwezo wa kitaaluma wa vijana waliomaliza shule za sekondari na vyuo kuwapa kazi ya kusomesha mitaani kwa ujira wa kujikimu, tofauti na mshahara wa kawaida ila una uhakika, tofauti na kubangaiza kutafuta kazi.

Ili serikali iweze kupata fedha za kukodisha kwa bei poa (kwani ni majengo au sehemu za wazi ambazo hazitumiki kwa sasa) itabidi iangalie upya mifumo ya ajira na mishahara au marupurupu serikalini, na pia idadi ya waajiriwa katika sekta tofauti, ili kuokoa fedha.

Ina maana kuwa uwezo wa waliojiriwa serikalini kupanga maslahi wanayotaka (hali ambayo ilipungua sana baada ya kuingia awamu ya tano) utapungua zaidi, kwani elimu ndiyo urithi ambao wazazi wanawapa watoto wa wakati huo. Vijana wanakuwa wasindikizaji huku wakijiandaa kuchangia jukumu hilo, kwani sasa haliachiwi familia.

Suala la kupanga upya umuhimu wa elimu katika mfumo mzima wa jamii na raslimali siyo la nafasi peke yake ila linaonekana hata katika kufungua shule zenye kidato cha sita, kuacha vyuo na vyuo vikuu. Baada ya shule kadhaa kutoa matangazo kuwa wanafunzi waje na vifaa au bidhaa zinazoweza kutumika endapo kuna tatizo la maambukizo ya corona, kama malimau, tangawizi na vinginevyo, wizara ilikataa jambo hilo kabisa. Ilisema ni kazi ya shule kuhakikisha hilo, ambayo ni sawa na kusema ni Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) ndiyo ihakikishe vifaa vya afya na visaidizi muhimu endapo tatizo linazuka. Wizara hiyo haitakuwa imejipanga kwa suala hilo na hapo kuna mkanganyiko.

Yako matazamio maeneo mengi duniani kuwa inaweza kupatikana chanjo ya corona hadi kufikia mwaka huu na kufanyiwa majaribio kwa makundi ya watu kuona kama inaweza kuzuia Covid-19.

Ila wanataaluma wanatofautiana kuhusu uwezekano huo kwani yako magonjwa yanayofanana na Covid-19 (homa kali ya mapafu) bado hayana chanjo. Ni maradhi ambayo yapo kuanzia 2012 (SARS) na 2014 (MERS) ilioripotiwa Mashariki ya Kati, ila ni yote ni shida ya kupumua kama ilivyo homa ya 'serious acute respiratory syndrome.' SARS pia ilianza wakati virusi vya wanyama pori wanaoliwa China vilipoingia kwa binadamu, hali ambayo pia ni chanzo cha ugonjwa wa ebola uliojikita zaidi Congo, ambao pia wanadaiwa kula sokwe.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU



Mnyama dugong, papa potwe na ngadu wanaotoboa minazi ni moja ya vivutio maarufu ndani za hifadhi bahari, **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Kasa kutamia, ngadu mitini, ni maajabu hifadhi baharini

Ni kawaida kuona hifadhi za wanyama pori, mapori tengefu na ardhi oevu vyote vikiwa vimehifadhiwa na kulindwa na serikali vyote vikiwa juu ya ardhi.

Lakini ni kwa nadra kusikia au kuona hifadhi ya viumbe bahari kama ilivyozoeleka kwa wanyama pori walioko Serengeti au Mgorongoro.

Hata hivyo, chini ya bahari nako zipo hifadhi za viumbe bahari, kuanzia mimea, wanyama, ndege na wadudu wa aina mbalimbali, ambao pengine hawalindwi na askari wa wanyama pori kama ilivyoeleka kwenye hifadhi za ardhini.

Tanzania Bara inaelezwa kuwa na hifadhi za viumbe bahari 18. Sehemu hizi kitaalamu huitwa Marine Protected Areas (MPAs), kwa mujibu wa Dk. Albogast Kyamukuru, mtaalamu wa elimu ya viumbe maji. Dokta Kyamukuru ambaye alifanya utafiti wa shahada za uzamivu katika kisiwa cha Mafia ambayo ni moja ya hifadhi maarufu ya bahari duniani, kwa miaka mingi kabla ya kustaafu alikuwa mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe kuhusu hifadhi za bahari anasema hifadhi hizo ni Kisiwa cha Mafia maarufu kama Mafia Island Marine Park, kuna kisiwa cha Nyororo, Mbarakuni na Shungimbili vyote viko wilayani Mafia mkoa wa Pwani.

Kamukuru anataja hifadhi nyingine kuwa Mnazi Bay Ruvuma inayopatikana Mtwara, wakati mkoani Tanga ziko kadhaa kama oelacantha iliyoko Muheza na kuna Kisiwa cha Mwewe.

Jijini Dar es Salaam, msomi huyu wa viumbe bahari anasema kuna hifadhi ya kisiwa cha Bongoyo, Fungu Yasini, kisiwa cha Mbudya, Pangawee, Sinda, Kendwa na Makatube

"Mafia Island Marine Park ndiyo kubwa kuliko zote hapa Tanzania. Ilianzishwa mwaka 1995 kufuatia sheria ya kuhifadhi viumbe bahari iliyotungwa mwaka 1994. Ina eneo kubwa kuanzia rasi ya Chole (Chole Bay) na eneo la hifadhi ya matumbawe ya Kitutia ( Kitutia Reef marine reserves...)" anaeleza.

> Whale shark au potwe ni miongoni mwa samaki wakubwa wenye zaidi ya mita 12 ambaye anapatika kwa misimu kwenye hifadhi ya Mafia. Ndiyo maana hifadhi hii ya bahari ni muhimu kwa taifa na duniani pia.



### UMUHIMU WA HIFADHI

Mtaalamu huyu anasema hifadhi ya bahari ni muhimu kwani ndilo eneo linalowezesha kupatikana taarifa za kiikolojia ya bahari na viumbe hai.

Lakini, pia kuna ekolojia ya mimea ya mwambao mikoko , matumbawe, mimea ya bahari, (sea grass) na kadhalika misitu ya mwambao.

"Kuna viumbe bahari wa kipekee kwenye hifadhi ya Mafia yuko mnyama bahari aitwaye 'dugong' anayeishi kwa kula nyasi. Ni miongoni mwa wanyama walio kwenye hatari ya kutoweka dunia akitajwa na shirika la kutetea wanyama waliokatika hatari ya kutoweka la CITES." Anasema mtaalamu.

Anaongeza kuwa hifadhi ya Mafia imejaa aina tano za kasa (kobe wa bahari) wenye viota ambao hutamia mayai kwenye mchanga ufukweni.

"Whale shark au potwe ni miongoni mwa samaki wakubwa wenye zaidi ya mita 12 ambaye anapatika kwa misimu kwenye hifadhi ya Mafia. Ndiyo maana hifadhi hii ya bahari ni muhimu kwa taifa na duniani pia." Anaeleza.

Anasema kitaaluma wasomi na watafiti wanatumia hifadhi hii kujifunza masuala ya bayoanuai za bahari na kuchangia elimu na utaalamu zaidi wa kuendeleza sayansi za viumbe bahari.

Aidha, Dk Kamukuru anasema kuwa Kisiwa cha Mafia kinachangia kiwango kikubwa cha samaki wanaouzwa soko la Ferry jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa wataalii ni sehemu inayofikiwa na watalii wanaozuru viumbe adimu vya bahari, kuogelea na kuangalia papa potwe 'whaleshark,' kuvua na kwa ujumla ni eneo linalovutia wageni, watafiti na wawekezaji.

### HIFADHI D'SALAAM

Dar es Salaam nayo ina hifadhi za Bahari za Dar es Salaam (DMRS) zinahusisha visiwa saba vya Bongoyo, Pangavini, Fungu Yasin, Mbudya Sinda, Makatobe na Kendwa.

Kwa mujibu wa mtandao hifadhi hizo zina sifa lukuki mojawapo ni uwapo wa ndege weupe wanaoonekana sehemu mbalimbali jijini, mwambao na ndani ya bahari.

Ndege hao mara nyingi jioni hurejea kwenye viota vyake visiwani humo. Kwenye visiwa ndiko yaliko makazi na mazalia ya ndege hao wenye rangi nyeupe na shingo ndefu zenye ufito mweusi unaoambaa hadi kichwani.

Ndege hawa wakati mwingine huruka kwa makundi juu ya bahari na wanaweza kutumiwa na wavuvi kuainisha sehemu yenye samaki wengi.

Aidha, kuna viumbe bahari kama kaa maarufu kama 'coconut crab', ambaye hujishikiza kwenye minazi, aidha wapo kasa na mimea mingi inayopatikana mahsusi maeneo eneo hayo licha ya kwamba ni sehemu zenye hoteli na miundombinu ya kuvutia watalii.

Kwa ujumla hifadhi za Dar es Salaam zinafikika lakini za Mafia licha ya uzuri wa kipekee zina changamoto ya usafiri.

Mafia kuna vivutio vya kipekee na hifadhi bahari hiyo inayotembelewa pengine kuliko za Dar es Salaam kwa miaka mingi haifikiki kwa urahisi kwa vile hakuna boti ya uhakika ya kuwafikisha watalii na wasafiri wengine kisiwani humo.

Njia pekee ya kufika Mafia ni kwa kutumia ndege ambazo wakati mwingine ni za kukodi, hivyo uzuri wa eneo hilo unabakia kusikika zaidi kuliko kuonekana hasa kwa wasioweza kumudu gharama.

Licha ya kuwapo wanyama na viumbe bahari wa kipekee ni sehemu yenye nazi nyingi zenye ladha ya mujarabu, na samaki wengi wakubwa, pweza, ngisi na kamba wakiwamo koche (lobsters) na 'prons' hata hivyo licha ya kufikishwa Dar es Salaam na mikoani bei zake ni kubwa kutokana na gharama za usafiri inayochangiwa na ukosefu wa miundombinu hasa meli na barabara.

Wakazi wa Mafia wanatumia mitumbwi na majahazi kusafiri kutoka kisiwa kimoja kwenye kingine.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Mafia Shaibu Nnunduma, tatizo la usafiri linaelekea kufikia ukingoni wakati wowote kuanzia sasa.

Akirejea ahadi ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ambaye mwishoni mwa mwaka jana alitangaza kuwa wilaya hiyo Februari mwaka huu ingepata meli anasema usafiri utakuwa wa uhakika.

Anasema meli hiyo itasafirisha abiria na shehena kutoka bandari ya Nyamisati iliyoko wilayani Kibiti hadi kisiwani Mafia.

Abiria wakifika Nyamisati watasafiri maeneo mengine kwa kutumia barabara inayoelekea mikoa ya Lindi na Mtwara

Nnunduma anaeleza kuwa jitihada zinaendelea na meli hiyo huenda ikiaanza kazi wakati wowote mwezi huu.

SAYANSI

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Misitu inavyotikisa maabara zinazosaka tiba ya corona

MOJA ya vitu muhimu duniani sasa ni misitu na mimea mbalimbali ambayo ni hazina kuu kwa binadamu na ulinzi wa mazingira ardhini na angani.

Kwa mfano mapafu ya dunia au misitu kama Congo au Amazon, ndiyo inayoondoa gesiukaa angani na kuingiza gesi ya oksijeni ambayo inatumiwa na binadamu na viumbe wengine kwenye michakato muhimu ya maisha.

Ni kazi inayofanywa na mimea au misitu na ndivyo inavyotimiza jukumu la kusafisha hewa. Utafiti na machapisho mbalimbali yanafahamisha kuwa misitu na mimea ni chanzo muhimu cha dawa duniani.

Aidha, uzoefu na matumizi vinaonyesha kuwa mimea huota na kukua na katika mchakato huo huwa inadhurika na hata kupatwa na magonjwa kupitia vimelea na fangasi.

Katika hali hiyo ustawi wa misitu na mimea hudhoofika lakini hujitibu kwa namna moja au nyingine katika mazingira yake.

Ni jinsi gani hali hiyo hufanyika inabakia kitendawili ambacho Mungu ambaye ni tabibu mkuu alikiweka tangu uumbaji maana aliumba kwa ufanisi.

Kadhalika, mwili wa binadamu nao uliumbwa ukiwa na uwezo wa kupambana na magonjwa mbalimbali kupitia mfumo wake wa kujikinga. Jamii za vizazi vilivyotangulia ziliishi kwa afya kwa miaka mingi kwa kutegemea nguvu zao za miili.

Hali iliyoimarishwa kupitia mfumo wao wa kuishi kwa kufanyakazi wakitumia nguvu ya mwili na kula vyakula sahihi kuujenga mwili na iwapo itatokea kutojisikia vizuri walitumia dawa za mimea.

Mambo yalianza kubadilika maendeleo yalipoanza kuchukua nafasi yake na ugunduzi kuanza kupitia mapinduzi ya viwanda.

Mifumo ya kufanyakazi ilianza kuwa tofauti kadhalika, namna ya kuishi na vyakula vilivyotumika kwa kutozingatia umuhimu wa lishe bora kwa minajili ya kuimarisha nguvu za mwili. wMaendeleo ya viwanda yalihusisha pia utengenezaji dawa kupitia viwanda na katika mwelekeo huo umuhimu wa misitu na mimea kama vyanzo muhimu vya dawa ulizingatiwa.

Kwa kutambua hali hiyo wataalam walijikita katika kutafuta miti na mimea yenye vinasaba vya kutibu magonjwa mbalimbali.

Aina nyingi za miti na mimea zilikusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kina kisayansi na hatimaye kupata aina zinazofaa kwa dawa.

Kupitia viwanda utengenezaji wa dawa ukaimarika hasa kwa kutumia vinasaba vya kutibu na kutokomeza vimelea au kupunguza nguvu ya virusi na kuanza kutengenezwa kwa vingi na viwanda vya dawa kuimarika.



Mmea ni chanzo cha dawa, huliwa na watu kabla ya kusindikwa viwandani na pia hutumiwa inapochunguzwa kimaabara na kutengenezwa dawa za kila aina. **PICHA: MTANDAO**



Inaaminika kuwa asilimia 75 ya dawa zinazotengenezwa duniani asili yake ni misitu, miti na mimea.

### VIRUSI VYA CORONA

Sasa COVID-19 imevamia dunia na mabara zote zimezingirwa na virus vya corona ambavyo ndicho chanzo cha COVID-19 vinavyoelezwa kuwa ni ugonjwa uliozuka Desemba, 2019.

Hii ni kutokana na corona kuanzia China kwenye jimbo la Hubei ndani ya jijini la Wuhan na kusambaa dunia nzima.

Mpaka sasa ugonjwa huu ni hatari kwa uhai wa binadamu hakuna chanjo wala dawa ingawa tunasema baadhi ya mitishamba inasaidia kuimarisha nguvu za mwili hivyo kupambana na COVID-19 na hatimaye wagonjwa kupona.

Itakuwa faraja kubwa iwapo chanjo au dawa ikaweza kupatikana kutokana na rasilimali misitu na mimea.

### MIMEA TIBA

Mimea na miti inachangia sana kwenye maendeleo ya viwanda dawa. Hivyo yawezekana COVID-19 ikapata udhibiti kutokana na nguvu za miti na mimea.

Naviangalia virusi vya corona kama kitu cha ajabu ambacho hata mwanzo wake haujulikani kiuhalisia. Hii inatokana na jinsi virusi hivyo vilivyosambaa kwa kasi kubwa na kwa dunia nzima na kusababisha maafa makubwa kiuchumi, kiafya na kijamii.

Ajabu kirusi hiki kimekuwa tishio kwa maisha katika mataifa yaliyoendelea zaidi yenye mifumo bora na kisasa katika sekta ya afya lakini pia kiuchumi.

Nchi za uchumi mdogo za Afrika Kusini ya Sahara, ikitokea hali kama ilivyoripotiwa Ulaya na Marekani wasingeshangaa maana inafahamika kuwa wanaishi ndani ya mifumo dhaifu ya kiafya na uwezo mdogo kiuchumi.

Hivyo kwa magonjwa kama malaria, kipindupindu au kuhara yamekuwa ya madhara lakini watu wanaishi.

Lakini 2020 imezuka COVID-19 ambayo haina matibabu ya kuaminika lakini Afrika imepambana nao kikamilifu kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu aliye muweza wa yote na tabibu namba moja aliyeumba viumbe ni kuvipa mfumo wa jeshi la kinga unaovizuia kupambana na magonjwa na kuyadhibiti, kwake hakuna lisilowezekana.

Ndiyo maana nguvu zetu zinaelekezwa kwanza kwa Mungu muumba wetu na pili, katika kupambana kuzuia maambukizo ya COVID-19 yasisambae sana mijini na vijijini.

> “Ajabu kirusi hiki kimekuwa tishio kwa maisha katika mataifa yaliyoendelea zaidi yenye mifumo bora na kisasa katika sekta ya afya lakini pia kiuchumi.

### TAHADHARI MUHIMU

Kila mmoja achukue tahadhari kikamilifu, kuvaa barakoa muda wote, kunawa mikono mara kwa mara kwa maji yanayotiririka pamoja na sabuni.

Aidha, ni lazima kutumia vitakasa mikono (sanitizer), kuepuka misongamano isiyo ya lazima; kutoshikana mikono au kukumbatiana, kujifunika kwa kitambaa safi au sehemu ya mbele ya kiwiko cha mkono wakati wa kupiga chafya au kukohoa.

Kadhalika kutulia nyumbani iwapo hakuna shughuli muhimu ya kufanya nje ya nyumbani ya lazima na muhimu ya kukupeleka kwenye mikusanyiko.

Vilevile, hatua zitakazochukuliwa kama za kisera na udhibiti zilenge kuimarisha usalama wa chakula na lishe maana miili ikiendelea kuwa dhaifu ndipo COVID-19 itapata nguvu.

Pia suala la upatikanaji maji safi na salama ni jambo la msingi sana. Kadhalika, vita yetu kwa COVID-19 iimarishwe kwa kutumia matibabu asilia kupitia mitidawa kama kujifukiza lakini kwa njia sahihi na kwa wakati muafaka na isiwe kiholela.

***Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki mstaafu.***

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Licha ya corona Makumbusho Kidijitali yang'ara D' Salaam



Biashara ya utumwa ni moja ya mambo yaliyoidhalilisha Afrika kwenye karne ya 17, vielelezo vyake vipo Makumbusho ya Taifa. **PICHA: MTANDAO**

MAADHIMISHO ya Siku ya Makumbusho Duniani yalianzishwa na Baraza la Makumbusho Duniani (International Council of Museums - ICOM) mwaka 1977 kwa lengo la kujenga uelewa kwa jamii kwamba taasisi hiyo ina muhimu kipekee.

Ndilo eneo ambalo urithi wa asili na utamaduni unahifadhiwa na jamii kubadilishana utamaduni hai kwa mazingira ya sasa.

Siku hiyo ya makumbusho ni muhimu kwani ina nguvu ya kuleta utengamano na jamii na kujenga umoja wa kitaifa, uzalendo na kufanya watu kuelewana zaidi.

Aidha, huleta kuthamini na kuhifadhi urithi wa asili na kiutamaduni kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

Siku hiyo huadhimishwa kila mwaka Mei 18, ambapo makumbusho zote duniani hufanya shughuli mbalimbali zenye lengo la kupeleka elimu kuhusu umuhimu wa makumbusho kwa wananchi.

Sherehe hizo huambatana na maandamano na shamra shamra za kila namna. Katika siku hiyo makumbusho zote duniani zinakuwa wazi kwa wananchi kuingia na kutoka bila kulipia gharama za kiingilio ili kujionea kazi mbalimbali.

Mirindimo ya maadhimisho hayo kwa mwaka 2020 nchini na duniani kwa ujumla imekuwa tofauti kwa sababu ya janga la ugonjwa wa korona ulioikumba duniani yote.

Kama moja ya njia ya kujikinga na maradhi huo mikusanyiko hairuhusiwi na jamii inahimizwa kuwa na tahadhari ili kuepukla corona. Kaulimbiu ya maadhimisho mwaka huu ni Makumbusho kwa Usawa, Anuai na Ushirikishwaji (Museum for Equality: Diversity and Inclusion).

Wakati dunia ikiadhimisha Siku ya Makumbusho Duniani, baadhi ya nchi zimefunga shughuli za kimakumbusho kwa muda ili kupisha janga la corona.

Kwa upande mwingine, Tanzania inaungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha siku hiyo kwa kutekeleza maelekezo ya serikali na Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kupambana na ugonjwa wa corona kupitia onyesho la kigitali liitwalo "Makumbusho Salama".

Katika uzinduzi uliofanyika siku hiyo inaonyesha ni jinsi gani Makumbusho ya Taifa yamejizatiti katika kudhihirisha kuwa kila anayeyatembelea anakuwa salama.

Sambamba na huduma kwa wageni zinazoendelea kutolewa kwa tahadhari, Makumbusho ya Taifa, imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi hususani kufanya utafiti, kukusanya mikusanyo, kuhifadhi, kuelimisha jamii kwa njia ya maonyesho, semina na programu za

> "Tumechukua kila tahadhari kulingana na maelekezo ya Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa kila mgeni anayetembelea anaingia akiwa salama na anatoka akiwa salama pia.

kielimu juu ya masuala mbalimbali kuhusu urithi wa asili na utamaduni wa taifa kwa lengo la kurithisha, kutoa elimu na kuburudisha.

Akizungumza katika uzinduzi wa onyesho la "Makumbusho Salama", Mkurugenzi Mkuu wa Makumbusho ya Taifa, Dk. Noel Lwoga, anasema kuwa japokuwa kuna ugonjwa wa corona makumbusho zote zinaendelea kufanyakazi lakini tahadhari kubwa imewekwa ili kuwakinga watumishi wa makumbusho hizo pamoja na wageni wanaozitembelea.

"Tumechukua kila tahadhari kulingana na maelekezo ya Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa kila mgeni anayetembelea anaingia akiwa salama na anatoka akiwa salama pia", anasema Dk. Lwoga.

Kulingana na onyesho hilo hakuna mgeni anayeruhusiwa kuingia makumbusho bila kuwa na barakoa na akiingia tu anapimwa joto ili kujua hali ya afya yake.

Anatakiwa kunawa mikono na sabuni na maji yanayotiririka au kutumia vitakasa mikono huduma ambazo zipo katika kila mlango wa kuingilia na kutoka makumbusho.

Lengo la kutengeneza onyesho la kidigitali ni kuhakikisha ujumbe unawafikia watu wote si wale tu wanaoweza kutembelea makumbusho zetu bali hata wale walio nje ya nchi ili wajue Makumbusho ni salama, anasema Ezekiel Chance, Mkuu wa Idara ya Programu, Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam.

Anasema wananchi wanaweza kutembelea makumbusho zote bila kuwa na wasiwasi kwa sababu taasisi imechukua kila hatua stahiki kuhakikisha kuwa wanaotembelea wanakuwa salama.

Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) wa Makumbusho ya Taifa, Lusekelo Kaisi, anasema kuwa pamoja na maonyesho na programu za kielimu taasisi ya Makumbusho ya Taifa inaendelea kuimarisha mifumo yake ya mawasiliano ya ikiwemo tovuti na mitandao ya kijamii ili kuwawezesha wananchi na jamii kwa ujumla kupata taarifa mbalimbali za kimakumbusho kwa urahisi zaidi.

"Kupitia njia hizi za mawasiliano jamii inaweza kupata taarifa, machapisho na maonyesho kwa urahisi bila wao kufika makumbusho," anasema Kaisi.

### TIBA YA NYUNGU

Kama sehemu ya maadhimisho hayo, Kijiji cha Makumbusho kilichoko Kijitonyama jijini Dar es Salaam kiliandaa onyesho la mila na tiba asili ambapo wanajamii kutoka kabila la Wamakonde na Wafipa walionyesha jinsi ambavyo tiba za asili zilitumika kutibu magonjwa mbalimbali.

Kazi hiyo iliyokuwa mubashara katika mitandao ya kijamii ya instagram, facebook na youtube lilionyesha majani yanayotumika katika kujifukiza na jinsi ya kujifukiza kwa magonjwa mbalimbali yakiwamo mafua makali, kichwa na tumbo.

Mkurugenzi wa Kijiji cha Makumbusho Dk. Gwakisa Kamatula, anasema Makumbusho ina hazina kubwa ya urithi wa utamaduni. Anaeleza kuwa ukiachilia mbali uhifadhi wa nyumba za asili za jamii mbalimbali za Tanzania, Kijiji cha Makumbusho kinahifadhi msitu wa asili wenye ukubwa wa takribani heka tano wenye miti na mimea mbalimbali ambayo inaweza kutumika katika tiba asili.

"Tupo hapa kwa lengo la kutoa elimu kwa jamii juu ya matumizi mazuri ya tiba asili hususan suala zima la kujifukiza" anasema Dk Kamatula.

Mary Mangazini kutoka kabila la Wafipa anasema katika jamii yao kujifukiza siyo jambo geni kwa sababu kunatumika sana kwa magonjwa mbalimbali ambapo majani ya mwarubaini, tangawizi pori, mpera, mkaratusi hutumika.

Anasema majani hayo huchemshwa kwa pamoja kwenye chungu kwa muda wa dakika 20. Maji hayo huipuliwa na kuwekwa pembeni kisha mgonjwa hufunikwa na nguo nzito (shuka au blanketi) kulingana na uzito wa mgonjwa.

"Akiwa mnene anatakiwa atumie nguo nzito zaidi ukilinganisha na mtu mwembamba" anasema Mangazini. Anasema mgonjwa anatakiwa kujifukiza kwa muda wa dakika tano mpaka 10 kutegemeana na ukubwa wa tatizo lake.

"Tiba hii ni rahisi sana na mara baada ya kujifukiza mgonjwa hupata nafuu au kupona kabisa," anaeleza Mangazini.

### KUOMBEA TAIFA


Nayo Makumbusho ya Majimaji Songea ilitumia maadhimisho hayo kuombea nchi dhidi ya ugonjwa wa corona.

Baraza la Kimila la Songea kwa kushirikiana na wanajamii walifika katika kaburi la halaiki la mashujaa wa vita vya Majimaji kuiombea nchi dhidi ya janga hilo.

### UTALII NDEGE

Makumbusho ya Elimu Viumbe Arusha walitumia maadhimisho hayo kuzindua programu ya ushirikishwaji wa vijana kwenye makumbusho hususani kupitia vikundi vya vijana vya utazamaji na utalii wa ndege katika mkoa wa Arusha.

Kaimu Mkurugenzi wa Makumbusho ya Elimu Viumbe Christine Ngereza, anasema kuwa vijana ni kundi muhimu katika suala zima la uhifadhi, hivyo, ni muhimu washirikishwe ili kujenga uelewa na uzalendo.





# Wamwomba Rais maeneo ya biashara stendi mpya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA ndogo na mamalishe zaidi ya 100 katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, wamemwomba Rais John Magufuli, kuwasaidia kupata nafasi ya kufanyia biashara zao, baada ya halmashauri kushindwa kuwapa kipaumbele kwenye ugawaji wa maeneo katika stendi mpya ya mabasi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, mmoja wa wafanyabiashara ambao kwa sasa wapo katika stendi ya muda ya Nanenane, Emanuel Kamboya, alisema kuwa waliahidia na halmashauri hiyo kuwa wao ndiyo watakaopewa kipaumbele baada ya stendi hiyo kukamilika.

Kamboya, alisema awali walihamishwa kutoka eneo iliyokuwa stendi kuu ya mabasi eneo la mjini ambako Shirika la Reli nchini (TRC), ndiyo walikuwa wamiliki na kuondoa kupisha Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR).

"Awali tulikuwa tukifanya biashara katika stendi ya zamani ya mkoa ya kule mjini ambako tulivunjiwa vibanda vyetu baada ya TRC, kulichukua eneo lao na jiji wakatuamuru wote tuje huku Nanenane, katika stendi ya muda na baada ya kukamilika kwa stendi mpya sisi ndiyo tuliahidiwa kupewa kipaumbele," alisema Kamboya.

Alisema pamoja na kuahidiwa kuwa watapewa kipaumbele cha kupatiwa maeneo ya kufanyia biashara, hali imekuwa tofauti kwa kuwa waliopatiwa maeneo katika stendi mpya ni watu wengine tofauti na wao.

"Waliopewa ni watu tofauti kabisa na sisi ambao tulikuwa tunafanya biashara katika stendi ya kwanza iliyovunjwa, tumetafuta msaada katika maeneo mbalimbali kwa viongozi wetu tumeshindwa, hivyo sasa tunamwomba Rais Magufuli, atusaidie na sisi kupata maeneo kwa kuwa kuanzia leo (jana), stendi mpya inaanza kutumika rasmi," alisema.

Naye Tausi Maulidi, alisema lengo la kumwomba Rais Magufuli kuwasaidia ni kutokana na kukosa msaada kwa viongozi waliowalilia kilio chao.

"Sisi hapa tulipo hatuna kitu kingine cha kukitegemea kupata riziki yetu ya kila siku, lakini tuna mikopo ya kuendesha biashara zetu, tukikosa nafasi ya maeneo ya kufanya biashara tutakosa namna ya kuishi na familia zetu," alisema Maulidi.

Akijibu malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alikiri wafanyabiashara hao kuahidiwa na halmashauri kuwa ndiyo wangepewa kipaumbele.

Katambi alisema, kutokana na janga la corona, jiji liliamua kutumia mfumo wa kuomba maeneo kwa njia ya mtandao hali ambayo ili mlazimu kila mtu kuomba eneo kwa usawa bila kujali nani alikuwapo awali.

"Kweli hawa wafanyabiashara, waliahidiwa na jiji kupatiwa kipaumbele, lakini mfumo uliotumika sasa ulihusisha watu wote na wao pia walipaswa kuomba kama wengine, lakini nimeshaongea na watu wa jiji wakutane nao ili kuwaelimisha," alisema Katambi.

# Hasunga asisitiza vyama ushirika ulipaji mazao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema mfumo wa stakabadhi ghalani hauwezi kufanya kazi kwa ufanisi kwenye eneo ambalo hakuna chama cha ushirika, ghala wala mtu mwenye leseni kutoka Bodi ya Mazao.

Kufuatia hali hiyo, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuwaruhusu wakulima kuuza mazao yao wanapoona inafaa bila kubugudhiwa.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki kufuatia baadhi ya wakulima wa Wilaya za Dodoma kulalamikia mfumo huo.

Hasunga alisema mahali popote kusikokuwa na chama cha ushirika vilivyoanzishwa na wananchi wenyewe wala maghala yaliyosajiliwa, hakuna wenye leseni wanaotambulika na bodi ya mazao, huu mfumo wa stakabadhi ghalani hauwezi kufanya kazi kwa ufanisi.

"Wananchi wasibugudhiwe waruhusiwe kuuza wanapoona inafaa, kwa sababu kulima wanaamua mwenyewe na kuuza wauze wenyewe," alisema.

Alisema kama mzigo unazidi tani moja lazima kodi za halmashauri zilipwe.

"Katika huu mfumo wakuu wa mikoa na wilaya sio wasimamizi, vyama vya ushirika vinasimamiwa na bodi ya mazao inakuwapo pale ndio wanafanya minada, wakuu wa mikoa kazi yao ni kusimamia kuhakikisha biashara inakwenda vizuri," alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakulima Wilaya ya Chamwino, waliomba serikali kuwawezesha kuanzisha vyama vya msingi kabla ya kuanza kutumika kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye zao la ufuta.

Mkulima Ndabazi Hamisi kutoka kijiji cha Manda, alisema katika zao la ufuta kama hakuna viongozi wao wa kijiji wanaowafahamu ni vigumu kuuza mazao yao. "Mimi nafikiri wangeanza na kuanzisha vyama vya msingi kwa mfano Manda kungekuwa na chama cha msingi na ghala lao lenye bima, kwa sababu ghala wanalopeleka Fufu, hatujui kama lina bima," alisema.

"Ninapouza mazao yangu nataka fedha nipewe hapo hapo, lakini inapokuja mfumo huu unasema ukishapima fedha hadi ndani ya wiki mbili ndio unapewa wakati mimi nina shida, sina raha bora wangekuja tujadiliane kama ni fedha taslimu kwa bei watakayokuwa wamepanga na wanatulipa hapo hapo, sisi tunataka hela."

Kwa upande wa wakulima wa Bahi, walisema sera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa vyama vya ushirika kila kijiji kiwe na ghala na kiongozi wa chama cha ushirika huku wakidai kuwa kwenye wilaya hiyo hakuna.

"Hakuna chama cha ushirika hata kimoja wilayani kwetu taarifa zilizopo kuna mtu hata hatumjui, tunapeleka tu mzigo barabarani na kuwekwa kwenye miti na hakuna ghala, wilaya nzima kuna ghala moja na hatuwezi kupeleka huko kwa sababu hatuna fedha ya kusafirishia," alisema mmoja wa wakulima, Nasibu Mohamed.

Naye, Mkazi wa Kondoa, Abeid Said alisema Mei 24, mwaka huu, wakati akielekea Dodoma mjini kuuza ufuta wake akiwa katika geti la Kidoka mzigo wake ulishushwa kwa maelekezo kuwa zao hilo linatakiwa kuuzwa kwa mfumo wa huo, jambo ambalo linampa wakati mgumu.

"Mimi nimelima nataka niuze mazao yangu ili nipate fedha, leo nashushwa kwenye gari mzigo wangu unachukuliwa napewa risiti, sijui mzigo huo unapelekwa wapi, nyumba tunazoishi zina panya hiyo risiti ikipotea haki yangu nitaipata wapi?" Alihoji.



Maofisa kilimo wa kampuni ya Tanzania Breweries Ltd (TBL) na wengine kutoka Shirika la Chakula Duniani (WFP), wakikagua moja ya ghala la kuhifadhi mtama mweupe katika Kijiji cha Chipogolo, wilayani Mpwapwa, mkoani Dodoma juzi. Kampuni ya TBL wananunua zao hilo, kwa bei ya 550/- kwa kilo moja, bila kutumia madalali. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Jamii yaombwa kusaidia makundi maalumu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAMII imeshauriwa kuendelea kuyasaidia makundi yenye uhitaji maalum ili kukidhi mahitaji yao muhimu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alipokuwa akigawa maziwa yaliyotolewa na Bodi ya Maziwa kwenye kituo cha kulelea watoto cha Kijiji cha Matumaini, jijini hapa.

Alisema bodi hiyo imefanya jambo zuri kwa sababu maziwa yatasaidia kuwatengenezea watoto lishe kijiji cha Matumaini, vituo vya afya na hospitali ambazo zimepata mgao huo.

"Unaweza kuona jitihada zinazofanywa na Kijiji cha Matumaini, umri wanaowachukua watoto ni kuanzia mwaka sifuri mpaka wa mtu mzima sio jambo jepesi, watoto wana mahitaji mengi na makubwa, ni watoto wasiokuwa na wazazi," alisema.

Aliziomba kampuni nyingine ziendelee kusaidia watoto walio katika mazingira magumu wanatunzwa kwa kupewa vyakula vya lishe hasa kipindi hiki cha kukabiliana na maambukizo ya virusi vya corona.

Naye, Father Vicent kutoka Kijiji cha Matumaini aliishukuru bodi hiyo na serikali kwa kutoa msaada huo kwa watoto waliopo katika kituo hicho na wanaamini maziwa hayo yatawasaidia kuwaongezea lishe mwilini.

Alisema serikali kupitia taasisi zake imekuwa ikiwakumbuka mara kwa mara watoto yatima ambao wanatunzwa katika vituo mbalimbali vya malezi jambo ambalo linatia moyo.

"Tunamshukuru Mkuu wa Wilaya kwa kushiriki katika zoezi la ugawaji maziwa tunaomba na wengine wasisite kuja kutoa misaada kupitia taasisi mbalimbali," alisema Vicent.

Bodi hiyo imetoa lita 1,650 za maziwa kwa watoto wa Kituo cha Kijiji cha Matumaini, Kituo cha Afya cha Mkonze, Chigongwe na Hospitali ya Mkoa.

# UWSSA yakabiliwa ukata, upanuzi maji wakwama

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (UWSSA), imedai kushindwa kupanua huduma zake na kuwafikishia wananchi maji ya uhakika kwa sababu ya ukata unaosababishwa na baadhi ya wananchi pamoja na taasisi nyingi za umma kutolipa madeni ya ankara za maji yanayofikia zaidi ya shilingi bilioni nne.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa Bodi ya hiyo, Edina Mwaigomole, wakati wa kikao na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kilichokuwa na lengo la kusikiliza na kutatua matatizo mbalimbali yanayoikwamisha taasisi hiyo.

Alisema deni hilo la shilingi bilioni nne ni kubwa na limechangia kukwamisha shughuli za kupanua mtandao wa huduma ya majisafi na taka kwa wakazi wa Jiji la Mbeya.

"Mji unazidi kupanuka na huduma ya maji inahitaji, hili deni la bilioni nne lingesaidia kuboresha huduma za maji, tumejitahidi kuwakumbusha wadaiwa, lakini bado wanaomba tusubiri, tunaomba mkuu wa mkoa tusaidie kulisimamia hili," alisema Mwaigomole.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa UWSSA, Mhandisi Ndele Mengo, alisema uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na wizi wa maji unaofanywa na baadhi ya wawekezaji hasa wa hoteli kubwa jijini Mbeya ni mambo yanayoikosesha mamlaka yake mapato inayostahili.

Wizi wa maji ni miongoni mwa sababu zinazoikosesha mamlaka hiyo mapato kwa sababu baadhi yao hujiunganishia mtandao wa maji kinyemela na kiasi cha maji wanachokizalisha sicho kinachowafikia wateja.

Kufuatia hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya aliagiza wadaiwa wote wakatiwe huduma na wasirudishiwe hadi watakapolipa madeni yote.



Vijana wanaofanya kazi kwenye Taasisi ya Tulia Trust, wakisaidia kufanya ukarabati wa nyumba ya mjane Julieth Mswachi, Mkazi wa Iganzo, jijini Mbeya jana, ambapo taasisi hiyo, imeamua kuezua mabati yake yaliyokuwa yamechakaa na kuezeka mapya. . **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# Wakazi Mwatenga waomba kutengenezewa barabara

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKAZI wa Kata ya Mwatenga katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wameomba serikali kuwatengenezea barabara kutoka Igalako hadi Mwatenga ili waweze kusafirisha mazao yao kutoka shambani.

Wakizungumza jana na Nipashe, walisema ni miaka mitano sasa waliahidiwa kutengenezewa barabara hiyo, lakini hakuna kinachoendelea hali inayokwamisha usafirishaji wa mazao na kuleta hofu ya mazao yao kuibiwa shambani kwa sababu ya kukaa muda mrefu.

Zawadi Jackson, alisema kipindi cha mavuno ya mpunga wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ya hasara kutokana na tatizo la barabara wafanyabiashara wachache wanaofika.

Alisema, diwani wao anajitahidi kuikumbusha serikali ujenzi huo, lakini tatizo ni baadhi ya wataalamu kutoonyesha ushirikiano hali inayosababisha kuhisi kuna mgogoro kati yao na diwani.

Tabia Mvwango alisema, kinamama wengi wanajifungulia njiani wakiwa kwenye pikipiki kutokana na barabara kuwa mbovu na wengine kupoteza watoto.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwatenga, Hamisi Chawaka, alisema pamoja na kuwapo kwa ushirikiano baina yake na diwani, mkandarasi haonyeshi matumaini ya kuikamilisha barabara hiyo.

Alisema Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune, aliwaahidi kujenga barabara, lakini hadi sasa hakuna shughuli zozote za ujenzi zinazoendelea licha ya jitihada zao wanazozifanya ya kuchimba.

Diwani wa Mwatenga, Mashaka Sakunja, alisema mwaka 2019/2020, serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura), iliahidi kujenga kilomita saba na walianza na kilomita mbili katika Kijiji cha Mapogoro.

Aliwaomba wananchi kuendelea kuwa na subira kwa kuwa aliwasiliana na Meneja wa Tarura Mkoa na kuahidi kuendelea na ujenzi huo hivi karibuni baada ya mvua za masika kumalizika.

# Wafanyabiashara Mbeya wailillia TRA ulipaji kodi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Sido, jijini hapa wameiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kulegeza masharti ya ulipaji kodi kwa kutowafungia biashara zao wanaposhindwa kulipa kwa kuwa kipindi hiki biashara imekuwa ngumu kutokana na janga la Covid-19.

Waliyasema hayo jana wakati wakizungumza na Nipashe kuwa kipindi hiki biashara imekuwa ngumu kwa sababu hakuna wateja, hivyo TRA waangalie namna nyingine ya kukusanya kodi.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Lupakisyo Mwaipyana, alisema yeye ni mlipaji mzuri wa kodi, lakini kipindi hiki cha corona biashara kwake imekuwa ngumu kiasi cha kushindwa kulipa kodi kwa wakati.

Aliiomba TRA, kuanzisha utaratibu rafiki ambao utamsaidia mlipakodi kutoa fedha kidogo kidogo hadi hapo atakapomaliza deni lake.

Kwa upande wao wauza mitumba waliuomba uongozi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kupunguza utitiri wa ushuru sokoni hapo kwa madai kuwa umekuwa kero.

Meneja wa TRA Mkoa wa Mbeya, Eunice Mapunda, katika taarifa yake alisema mfumo wa ulipaji kodi kwa wafanyabiashara ni rafiki, hivyo wanapaswa kulipa kwa wakati.

Alisema TRA iliandaa utaratibu mzuri kwa mfanyabiashara yeyote kutoa taarifa kama anakabiliwa na tatizo lolote la kibiashara ikiwamo kupewa ushauri, hivyo kauli kwamba janga la corona imekuwa kikwazo ni ya kukwepa jukumu lao.

Aliwasisitiza wafanyabiashara wadogo na wajasiriamali kuchangamkia fursa ya vitambulisho vilivyotolewa na Rais kuvichukua ili kuondokana na adha ya kulipa kodi wasizostahili na kufanya biashara zao bila usumbufu.

**TRA iliandaa utaratibu mzuri kwa mfanyabiashara yeyote kutoa taarifa kama anakabiliwa na tatizo lolote la kibiashara ikiwamo kupewa ushauri, hivyo kauli kwamba janga la corona imekuwa kikwazo ni ya kukwepa jukumu lao.**

# Chumvi ya Pemba yapenya masoko ya Ulaya, Canada

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amesema chumvi inayozalishwa katika kisiwa cha Pemba imepata mafanikio na umaarufu kwa kuingia katika soko la Ulaya hadi Canada.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Balozi Amina, alisema hiyo ni hatua nzuri kwa wajasiriamali wazalishaji wa chumvi kutoka katika kisiwa cha Pemba kwa kuonyesha ubunifu wa usarifu wa uzalishaji huo.

Alisema chumvi hiyo yenye madini jote imepenya katika soko la dunia baada ya kusarifiwa kwa kuingizwa kwa baadhi ya mazao ya viungo ambavyo ni sehemu ya tiba.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tayari uzalishaji wa chumvi katika kisiwa cha Pemba kupitia Swahili Coast Salts umepata mafanikio makubwa na kuingia katika soko la Ulaya," alisema.

Aliupongeza uongozi wa kampuni ya Swahili Coast Salts chini ya mwekezaji wake, Stephanie Said, kwa kuonyesha uwezo wa ubunifu wa uzalishaji chumvi bora na kuingia katika ushindani wa soko la kimataifa.

Alisema mikakati ya Wizara ya Biashara ni kuimarisha sekta ya uwekezaji wa viwanda mbalimbali kuanzia vidogo vya wajasiriamali hadi viwanda vikubwa na hivyo kuongeza pato la taifa.

Alisema tayari vipo jumla ya viwanda saba ambavyo vimeanzishwa na wajasiriamali wazalendo katika mwaka 2019-2020, huku vikianza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali na kuingia sokoni.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawapongeza kwa dhati wawekezaji wazalendo kwa uwekezaji wao katika sekta ya viwanda vidogo vidogo, hivyo kuzalisha bidhaa mbalimbali na kusaidia kutoa ajira kwa wananchi," alisema.

Alisema Serikali ya Zanzibar imetenga jumla ya Sh. bilioni 6.85 kupitia kwa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SMIDA) kwa ajili ya kukuza viwanda na maendeleo ya wajasiriamali kupiga hatua kubwa ya sekta ya viwanda.



Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Said Hassan (kulia), akiteta jambo na Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana..**PICHA|: RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR**

# Kasi ya ubakaji yaishtua Tamwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa) Ofisi ya Zanzibar, kimesema kinasikitishwa na uwapo wa ongezeko la vitendo vya ubakaji.

Mkurugenzi wa Tamwa Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alitaka jamii wakiwamo wazazi, walezi, viongozi wa dini na vyombo vya sheria kusaidia kurekebisha tabia kwa watoto wa rika hilo la miaka 16, ambapo baadhi yao wanatuhumiwa kufanya makosa hayo.

Alieleza kuwa taarifa walizopata kutoka kwa wanaharakati wa masuala ya kijamii wamepokea mashtaka 10 katika shehia za Unguja na Pemba kuanzia Machi 17, mwaka huu ambapo matukio hayo yamefanywa na vijana wenye umri huo.

"Matukio hayo nane yametokea kisiwa cha Pemba na mawili katika kisiwa cha Unguja, yakiwamo kulawitiwa, kubaka na kutoroshwa," alisema.

Alisema Tamwa inaiomba serikali kuweka mipango madhubuti ya kubadilisha tabia ya vijana wa kiume ili kuruhusu wanawake na watoto kuishi kwa amani na kufikia malengo yao ya kimaisha.

Dk. Mzuri aliziomba mamlaka husika kuzishughulikia kesi hizo kwa haraka na kutoa adhabu zinazostahiki ili vitendo hivyo viweze kukomeshwa.

Naye Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Pemba, Makarani Ahmed, alisema katika kipindi hicho cha mlipuko wa corona kesi za matukio yote zinapokelewa ikiwamo kesi za udhalilishaji, lakini kunautaratibu wa kumfikisha mtuhumiwa mahakamani.

"Mkoa wa Kusini, Pemba imepokea kesi za udhalilishaji na zinaendelea na uchunguzi na tunapenda kuihakikishia jamii kuwa malalamiko yote yatapelekwa mahakamani pale ushahidi utakapokamilika pamoja na kuwapo kwa mapambano dhidi ya corona," alisema Makarani.

# Doria zanasa misumeno ya moto 77

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya misumeno ya moto 77 imekamatwa katika doria 246 zilizofanywa na Idara ya Misitu na mali zisizorejesheka, huku ikitumika kukata miti kinyume cha sheria.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ussi, aliyasema hayo wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu athari za mazingira na ukataji wa miti kwa kutumia misumeno ya moto.

Alisema tayari misumeno ya moto imepigwa marufuku nchini kutokana na kuwapo kwa athari za uharibifu wa mazingira, huku miti ya matunda ikiwamo minazi na miembe ikikatwa kiholela kwa matumizi ya mkaa na mbao.

Alieleza katika kipindi cha miaka miwili, zaidi ya minazi 200 imekatwa kwa matumizi ya mbao na mengine kupisha ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya wananchi.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wananchi kwamba misumeno ya moto imepigwa marufuku kutokana na kuongezeka kwa athari za uharibifu wa mazingira, ikiwamo kasi ya ukataji wa miti," alisema.

Alisema hivi sasa wapo watu wanavamia mashamba ya wananchi nyakati za usiku na kukata minazi kwa matumizi ya mbao.

"Tumepokea malalamiko mheshimiwa, wapo watu nyakati za usiku mashamba yao yanavamiwa na kukatwa minazi kwa matumizi ya mbao...sasa ndiyo maana tunapiga marufuku matumizi ya misumeno ya moto," alisema.

Alisema suala la kupiga marufuku misumeno ya moto halina mjadala kwa sababu ipo hatari kubwa katika siku za baadaye baadhi ya miti muhimu ikapotea na kizazi kijacho ikawa ni hadithi tu.

"Miti muhimu tayari hivi sasa imeanza kupotea kidogo kidogo kutokana na kasi ya ukataji wake kwa matumizi ya mbao na mkaa ikiwamo mizambarau, mibuyu na mifuu hivi sasa imepotea," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

District Land and Housing Tribunal Regulations
GN No. 174/2003
Form No. 2B
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IRAMBA
MAHALI - KIOMBOI – BOMANI
MAOMBI NA.04 MWAKA 2020
JUMANNE SEFU……………………….MUOMBAJI
DHIDI YA
FELISIAN AMA…………………MJIBU MAOMBI

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

KWA: FELISIAN AMA
WA ISHINSI KATA YA MSINGI

Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 18 mwezi wa 6 mwaka 2020 saa2.00 asubuhi mbele ya MH. B.J.SHUMA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 27 mwezi 05 mwaka 2020.

MWENYEKITI

157586

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)
Katika Mahakama ya Mwanzo NYANKUMBU

**Usimamizi wa Mirathi Na. 14/2020**

Ombi la **ANETH JOHN ZACHARIA** kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **GODIFREY FREDRICK METHOD**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/06/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 12/05/2020.

PRIMARY COURT MAGISTRATE
GEITA

157587

**TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**ELVIS KINYINA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T. 945 AHT AINA YA TOYOTA HILUX PICK UP.

KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

TAARIFA YA POLISI
**KAH/TR/RB/198/2020.**

157584

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA SHERIA
IDARA YA MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2

Katika Mahakama ya mwanzo ya Kinondoni
Usimamizi wa mirathi namna 92/2020
Ombi la John Richard Semkuya
Msimamizi wa mirathi ya marehemu Charles Richrd Semkuya.

Kwa: Yeyote anayehusika
Tanzania Bara.

Watu wote wanaodaiwa kuwa na husiano na Mirathi ya Marehemu huyo. Wanaalikwa kuja kuhudhuria Mahakamani kesi wakati wa kusikilizwa kesi mnamo tarehe 9/06/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hii.

Wosia wa Marehemu upo mahakamani waweza kukaguliwa.

NAKALA
Magomeni
Kariakoo
Kawe
Ilala
Mbagala
Temeke
Manzense
Kigamboni
Kimara.

157585

**ANATAFUTWA KUKAMILISHA SAINI**

Mimi **KULTHUM ABU MALLYA** wa Mbweni Malindi Estate, ninamtafuta Ndugu Sudi Halfan ambaye aliniuzia kiwanja mwaka 2012 chenye **No. CT49346 Plot No. 13 Block B** Mbweni Malindi Manispaa ya Kinondoni. Uje ukamilishe saini zako kwa hatua ya kubadili jina kuwa kwenye majina yangu.

Tafadhali wasiliana nami kwa namba ya simu: 0754 007 444.

157589

**MNAYA AUCTION MART COMPANY LIMITED**
P.O. BOX 80896, DAR ES SALAAM
Physical Address: Kibaha Tumbi EX, NBC House 1st Floor.

**Mnada Mnada Mnada**

Kampuni ya Mnaya Auction Mart kwa idhini tuliyopewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kibaha, itafanya mnada wa hadhara siku ya Alhamisi tarehe 04/06/2020, saa tano asubuhi. Tutauza nyumba iliyopo eneo la Kibaha kwa Mathias.

**Masharti ya Mnada**

1. Mnunuzi atatàkiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa
2. Màlipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kushindwa kufanya hivyo, mnunuzi atakua amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada kurudiwa.

**Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0718 925 291 au 0713 932 566.**

*Wote mnakaribishwa.*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo:
MJINI-MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;131/2020

Ombi la SEBASTIANA BENADICT NYIMBO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MARRY IDD PLANTAN.
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/06/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/06/2020.

157591

NIPASHE

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

## Mali alizopora Omar Bashir zaanza kufuatiliwa

**KHARTOUM,** Sudan

MAJENGO ya thamani ya mabilioni yaliyokuwa yakimilikiwa na utawala wa zamani wa Rais wa Sudan, Omar Bashir, yarudishwa mikononi mwa serikali, huku hatua kabambe za kuendelea kufuatilia mali nyingine nyingi ikifanyika.

Kamati ya kupambana na rushwa nchini humo iliyoanza kazi Desemba inaamini kupatikana kwa mali hizo ni mwanzo wa kazi kubwa inayofuata ya kuzirudisha mali nyingi zilizopo mikononi wa Bashir zilizopatikana kwa njia isiyokuwa sahihi.

Hata hivyo, wataalamu wanasema itakuwa vigumu baadhi ya mali kupatikana.

Msemaji wa kamati iliyopewa jukumu la kupambana na rushwa na kuuvunja utawala wa zamani nchini humo, Salah Manaa, alisema makadirio ya awali yameonyesha kwamba majengo na mali nyingine zilizomilikiwa na utawala huo wa zamani, thamani yake ni kati ya dola bilioni 3.5 mpaka nne.

Manaa aliliambia Shirika la Habari la AFP kwamba kilichoguswa hadi sasa ni sehemu tu ya vingi inapohusika mali jumla iliyopatikana kwa njia haramu na kufichwa chini ya utawala huo wa Bashir.

Omar Al Bashir aliitawala Sudan kwa mkono wa chuma kwa miaka 30, lakini aliondolewa kwa nguvu madarakani mnamo Aprili mwaka jana na jeshi la taifa hilo baada ya kufanyika maandamano makubwa ya wananchi walioupinga utawala wake.

Kamati hiyo mpya ya kukabiliana na rushwa na ufisadi nchini humo ilianza kazi Desemba mwaka jana na inawajibika mbele ya serikali ya kugawana madaraka kati ya raia na majenerali wa kijeshi iliyoundwa mnamo mwezi Agosti.

Kiongozi huyo wa zamani alishtakiwa na kuhukumiwa miaka miwili jela katika kesi mojawapo ya rushwa inayohusiana na umiliki wa fedha za kigeni kinyume cha sheria.

Ikiwa ni chini ya miezi sita tangu ilipoanza kazi kamati hiyo inazifuatilia kwa ukaribu mali za rais huyo wa zamani.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kamati hiyo ilipokea rundo la nyaraka zinazojaza malori matatu ambazo zote zitahitaji kupekuliwa na kuchunguzwa kwa makini. **DW**

# Wakili asema kifo cha George Floyd kilipangwa

**WASHINGTON,** Marekani

WAKILI wa familia ya George Floyd, Benjamin Crump, ambaye kifo chake kiliibua maandamano ya hasira kote nchini Marekani, amemshtumu ofisa wa polisi kwa "kupanga mauaji".

Wakili Crump alisema Chauvin na Floyd walikuwa tayari wanafahamiana kabla ya kifo chake.

Alisema kuwa familia ya Floyd ili fahamishwa kuhusu kifo chake na mmiliki wa klabu ambayo Derek Chauvin aliyekuwa polisi akilinda klabuni hapo, ambako pia George Floyd alikuwa mlinzi, kwa hiyo walikua wanapokezana.

Polisi wa Minneapolis, Derek Chauvin, ameshtakiwa kwa mauaji, lakini Wakili Crump amekiambia kituo cha habari cha CBS kuwa yalikuwa ni mauaji ya kiwango cha kwanza.

"Tunadhani kwamba alikuwa na nia... takriban dakika tisa aliendelea kushindilia goti lake kwenye shingo ya mwanaume ambaye alikuwa anamwomba amsamehe na kumwambia kuwa hawezi kupumua," alisema Crump.

Video kutoka katika vituo viwili vya televisheni vya Philadelphia Jumapili zilionyesha vijana wakivunja magari kadhaa ya polisi na kuiba katika duka moja.

**Ripoti ya uchunguzi ya West Philadelphia, imesema kuwa magari ya polisi pia yalichomwa moto. Miji kadhaa ya Marekani imeweka amri ya kutotoka nje.**

Ripoti ya uchunguzi ya West Philadelphia, imesema kuwa magari ya polisi pia yalichomwa moto. Miji kadhaa ya Marekani imeweka amri ya kutotoka nje.

Rais wa Marekani, Donald Trump alituma ujumbe wake wa twitter uliosema: "Sheria na amri vifuatwe Philadelphia, sasa wanapora maduka. Walete wanajeshi wetu waingilie kati".

Tukio la Floyd limeibua ghadhabu miongoni mwa Wamarekani juu ya mauaji yanayotekelezwa na polisi dhidi ya watu weusi.

Hii inafuatia kesi maarufu ya mauaji ya Michael Brown mjini Ferguson, Eric Garner mjini New York na kesi nyingine zilizowasilishwa mahakamani na vuguvugu linalojulikana kama Black Lives Matters.

Katika video, Chauvin alionekana akipiga goti kwenye shingo ya Floyd kwa dakika kadhaa, huku Floyd akisikika akisema kuwa hawezi kupumua. Maofisa wengine watatu walioukuwapo wakati wa tukio hilo pia wamefutwa kazi.

"Kutokana na ukweli kwamba ofisa wa polisi Chauvin aliendelea kushindilia goti lake kwenye shingo kwa takriban dakika tatu baada ya Floyd kupoteza fahamu hatuelewi kuwa hayo hayakuwa mauaji ya kiwango cha kwanza," alisema Crump na kuongeza:

"Hatuelewi ni kwanini maofisa wote hawa hawajakamatwa," wakili Crump alisema.

Kwa wengi ghadhabu ya kifo cha George Floyd pia inaonyesha hasira juu ya kutokuwapo kwa usawa na kuwapo kwa ubaguzi katika masuala ya kijamii na kiuchumi, ambao haupo Minneapolis pekee.

Kikosi cha wanajeshi wa ulinzi nchini Marekani- National Guard wa akiba kinachoshughulikia hali za dharura ndani ya nchi, kimesema jana kuwa wanajeshi wake 5,000 wamepelekwa katika majimbo 15 na Washington DC.

Katika mahojiano na kituo cha habari cha CBS, wakili Benjamin Crump alisema kwamba: "Sasa tuna sauti kutoka kwa polisi na tunasikia, ambapo polisi mmoja wao akisema hajatokwa na damu, labda tunaweza kumgeuza, lakini ofisa Chauvin anasema hapana, tutaendelea kumlaza hivi. Hiyo inaonyesha kuwa alifanya hivyo kwa makusudi.

"Na pia kwamba ofisa Chauvin aliendelea kushindilia goti lake kwa karibu dakika tatu baada ya George Floyd kupoteza fahamu." **BBC**



Mmoja wa waandamanaji nchini Marekani akionyesha kuchukizwa na kifo cha George Floyd kilichosababishwa na polisi. **PICHA: REUTERS**

# Mke wa Rais Nkurunziza aanza matibabu ya corona

**NAIROBI,** Kenya

TAARIFA kutoka Burundi zinaeleza kuwa mke wa Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza, Denisem yuko nchini Kenya akiendelea kupatiwa matibabu ambayo serikali ya nchi hiyo imesema siyo corona.

Katika taarifa ambazo zilianza kuenea jana jioni, zilieleza kuwa mke za Rais wa Burundi, yuko nchini Kenya, akiendelea kupatiwa matibabu ambayo Serikali ya Burundi inasema sio corona, huku vyanzo nchini Kenya vikithibitisha kuwa ni ugonjwa wa Covid- 19.

Shirika la Habari la Ufaransa, (AFP), lilimnukuu ofisa mmoja kwenye uwanja wa Melchior nchini Burundi, akithibitisha kuwa Denise alisafirishwa kwenda nchini Kenya na ndege ya shirika la kiafya AMREF.

Vyanzo katika wizara ya afya nchini Kenya, ambavyo havikutaka majina yao kutajwa vimethibitisha kuwa mke wa Rais Nkurunziza, yuko nchini humo akisumbuliwa na maradhi ya kupumua ambayo yanahusishwa moja kwa moja na ugonjwa wa corona.

Kuumwa kwa mke wa rais kunathibitisha hatari ya virusi hivyo nchini Burundi, taifa ambalo ni miongoni mwa nchi ambazo hazijatangaza makatazo ya watu kukusanyika wala kutembea kujaribu kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Wiki iliyopita nchi hiyo ilifanya uchaguzi wake mkuu, huku mikutano ya kisiasa ikishuhudia mamia ya watu wakijitokeza bila kuzingatia maelekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu kujikinga.

Awali Rais Nkurunziza alidai kuwa nchi yake haina haja ya kuweka makatazo kwa kuwa inalindwa na Mungu, akitupilia mbali madai ya hatari ya virusi vya corona. **RFI**

# IBRAHIMOVIC ASIFIWA KUTOKUWA MBINAFSI




**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic "hana ubinafsi" na amechangia makubwa pale Milan, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake, Hakan Calhanoglu.

Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, alirudi Milan Januari na amefunga mabao manne katika mechi 10 kabla ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mshambuliaji huyo kwa sasa anajiuguza maumivu ya kigimbi cha mguu kuelekea kuanza tena kwa msimu wa Serie A, huku majaliwa yake yakiwa bado hayajulikani.

Lakini Calhanoglu amemsifia sana Ibrahimovic, ambaye alishinda Serie A na Supercoppa Italiana wakati wa kipindi chake cha kwanza kuichezea klabu hiyo.

"Yeye ni mchezaji mpya wa Milan. Ni nyota wa dunia na ni mchezaji mwenye uzoefu mkubwa," alisema akiiambia beIN SPORTS.

"Yeye ni nyota wetu. Amechangia makubwa kwa timu na anaheshimika kwa uzoefu wake na malengo yake na ana msaada mkubwa dimbani."

Serie A ambayo ilisimama tangu Machi inatarajia kurejea tena Juni 20, mwaka huu.

# Sancho afungua 'lango' la hat-trick

**DORTMUND,** Ujerumani

NYOTA wa England, Jadon Sancho alifunga 'hat-trick' yake ya kwanza katika maisha ya soka tangu kurudi kwa msimu wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, wakati akisaidia Borussia Dortmund kuifumua Paderborn.

Baada ya kipindi cha kwanza, Thorgan Hazard aliiweka mbele Dortmund kabla ya Sancho kufunga bao lake la kwanza tangu Februari 29, mwaka huu.

Sancho aliongeza bao la tatu baada ya penalti ya Uwe Hunemeier kupunguza mabao kabla ya Achraf Hakimi na Marcel Schmelzer kila moja kufunga moja na ubao kusomeka 5-1.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, alikuwa Muingereza wa kwanza kufunga hat-trick kwenye ligi ya nje na nyumbani kwake katika ligi kubwa tano Ulaya kwa kipindi cha miaka 31 baada ya mshambuliaji wa Luton, Brian Stein kuwa mtu wa kwanza kufanikisha hilo, wakati akiichezea Caen dhidi ya Cannes kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Mei 31 mwaka 1989.

Baada ya kufunga bao lake la kwanza, Sancho alivua jezi yake na kuonyesha fulana ya ndani iliyoandikwa maneno "Haki kwa George Floyd". Floyd aliyekufa baada ya kufanyiwa unyama kwa kukanyagwa shingoni na polisi mjini Minneapolis, Minnesota nchini Marekani Mei 25, mwaka huu hadi kupoteza maisha.

Na baada ya mchezo huo, Sancho aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Najisikia fahari kwa 'hat trick' ya kwanza, ulikuwa wakati mzuri sana kwangu."

Bao lake la kwanza alifunga baada ya pasi kutoka kwa Julian Brandt, huku mchezaji huyo wa zamani wa akademi ya Manchester City akimalizia vizuri pasi ya Hazard na kufunga bao lake la pili.

Bao la tatu la Sancho kukamilisha 'hat-trick' na likiwa la 17 kwenye Bundesliga msimu huu, alifunga dakika ya 91 baada ya kukimbia na mpira kutoka winga ya kulia.







# *Depay mbeleko ya Lyon dhidi ya Juve*

**LYON,** Ufaransa

LYON itakuwa na faida kubwa kucheza dhidi ya Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama Memphis Depay atakuwa fiti, kwa mujibu wa kocha wa zamani, Sylvinho.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, walipata ushindi wa kushangaza wa bao 1-0 dhidi ya Juve kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 kwenye michuano hiyo Februari kabla ya msimu kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Depay mwenye umri wa miaka 26, aliukosa mchezo huo kwa sababu alikuwa majeruhi kutokana na kuumia tangu Desemba mwaka jana, lakini ameripotiwa kuwa anarudi kwenye mazoezi mwezi huu.

Sylvinho, ambaye alikuwa kocha wa Lyon katika mechi 11 msimu uliopita, anaamini mshambuliaji huyo anaweza kuisaidia klabu yake kupata ushindi kwenye mchezo huo wa pili.

"Lyon ilikuwa na matokeo mazuri nyumbani, lakini kumbuka kucheza nyumbani kwa Juventus ni ngumu sana kupata ushindi," alisema beki huyo wa kushoto wa zamani wa Barcelona na Arsenal akiiambia Sky Sport.

"Sijui kama Depay atakuwa tayari kurudi dimbani, lakini kama akifanikiwa, kwa hakika itakuwa tofauti sana. Ni mchezaji mwenye nguvu na akili.

"Nampenda sana. Kama atakuwapo kwenye mchezo huo itakuwa faida kubwa sana kwa Lyon."

Depay amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi 18 msimu huu na kurudi kwake kutaongeza nguvu kwa safu ya ushambuliaji ya Lyon, huku michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ikipangwa kumalizika Agosti.

# Icardi asajiliwa rasmi na PSG

**PARIS,** Ufaransa

MAURO Icardi amekamilisha usajili wa kudumu Paris Saint-Germain akitokea Inter Milan baada ya klabu hiyo ya Ligue 1 kuamua kumnunua moja kwa moja.

Icardi alihamia PSG kwa mkopo msimu uliopita baada ya mahusiano yake na viongozi wa Inter kutokuwa mazuri, na kurudi pale kwenye dimba la San Siro ilionekana kuwa jambo lisilowezekana.

Katika nusu ya msimu wa 2019-20 mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alikuwa na kiwango cha kuvutia na kumwondoa Edinson Cavani kwenye kikosi cha kwanza akitengeneza upatina mzuri na Neymar na Kylian Mbappe.

Hadi sasa amefunga mabao 12 katika mechi 20 alizocheza kwenye Ligue 1.

Mkurugenzi wa soka wa Inter, Piero Ausilio hivi karibuni alithibitisha kwamba PSG itamsajili Icardi ambaye mkataba wake ulikuwa unamalizika Mei 31, na sasa amesaini mkataba utakaomuweka kwa mabingwa hao wa Ufaransa hadi Juni 2024.

Ripoti zinadai kwamba PSG watalipa kwanza euro milioni 50, ambapo thamani ya mchezaji huyo ni euro milioni 57.






# BALOTELLI: MIMI SI MZIMU NISIONEKANE MAZOEZINI

**BRESCIA,** Italia

MARIO Balotelli amejibu ripoti kwamba alishindwa kuhudhuria mazoezi Jumapili, akisisitiza kwamba yeye si "mzimu" hadi asionekane kwenye kamera, kwani alikuwapo mazoezini.

Balotelli amekuwa akikabiliwa na wakati mgumu akiwa anacheza katika klabu ya mji wa nyumbani kwao ya Brescia, na nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, ameshafunga mabao matatu tu katika mechi 19 za Serie A msimu huu.

Rais wa Brescia, Massimo Cellino alisema Alhamisi kwamba anatarajia Balotelli kuondoka, akibainisha kwamba lilikuwa kosa kumsajili mshambuliaji huyo wa zamani wa Manchester City, ambaye aliripotiwa kukacha mazoezi ya Jumanne.

Pia vyombo vya habari vya Italia viliripoti Jumapili kwamba hakutokea kwenye mazoezi.

Hata hivyo, Balotelli alijibu tuhuma hizo kupitia ukurasa wake wa Instagram akikanusha madai hayo.

"Unawezaje kuandika vile kwamba sikuwapo uwanjani kwenye mazoezi? Kuna waandishi wengi wakati wote nikiwa kwenye mazoezi, tena na kamera zao za TV!" aliandika Balotelli kwenye Instagram.

"Nahudhuria mazoezi mara mbili kwa siku, karibia kila siku! Kwa nini mnakuwa hamna ushahidi? Sidhani kama nilikuwa mzimu, sionekani kwenye kamera."

# Schweinsteiger atabiri hat-trick mataji Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

BASTIAN Schweinsteiger anaamini Bayern Munich wamejipanga vema kushinda hat-trick ya mataji (makombe matatu) msimu huu wa Bundesliga, DFB-Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya soka kurudi tena.

Bayern tangu kurudi tena kwa Bundesliga baada ya kusimama kwa miezi miwili kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, imeshinda mechi zote nne ikiwamo dhidi ya wapinzani wao, Borussia Dortmund ambapo walishinda 1-0.

Kikosi hicho cha kocha, Hansi Flick kinaongoza msimamo kwa pointi 10 dhidi ya Dortmund na kitacheza na Eintracht Frankfurt kwenye fainali ya Kombe la DFB-Pokal, na wanaonekana wametanguliza mguu moja kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Chelsea.

Huku Bayern wakionekana kuwa na nafasi kubwa ya kulitwaa taji la Bundesliga, na bingwa mtetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Liverpool akiwa ashatupwa nje ya mashindano hayo, Schweinsteiger anafikiri klabu yake hiyo ya zamani ina nafasi ya kubeba mataji matatu.

"Ukilinganisha na timu nyingine za Ulaya, yenyewe ndio timu bora," alisema Schweinsteiger akinukuliwa na gazeti la Bild.

"Wanaweza kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, hasa kutokana na Liverpool tayari wameshatupwa nje ya mashindano.

"Kwenye DFB-Pokal wana mchezo wa nyumbani dhidi ya Frankfurt, naamini wana nafasi kubwa ya kushinda."

Schweinsteiger, alishinda mataji matatu akiwa na Bayern msimu wa 2012-13, alistaafu soka mwaka 2019 baada ya misimu miwili akicheza katika klabu ya Chicago Fire kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI ATABIRI SOKA TOFAUTI LA CORONA

●●● Itakuwa hali tofauti kabisa na ngeni kwetu, na kwa uhakika kabisa halitakuwa...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi anaamini soka kamwe halitakuwa tena sawa baada ya mlilipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu, Covid-19.

**Wakati Ligi za Ufaransa na Uholanzi zilifutwa rasmi msimu huu, ligi nyingine kubwa za soka Ulaya zinatarajiwa kuendelea mwezi huu, zikichezwa bila mashabiki.**

Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, ilirudi Mei 16 na Messi na Barca watarudi kumalizia msimu wa LaLiga, ambao unatarajiwa kuanza Juni 11.

Ligi Kuu ya England itaanza Juni 17, huku ile ya Italia, Serie A, ikipangwa kurejea Juni 20, mwaka huu.

Akizungumza na El Pais, Messi alisema: "Sidhani kama soka litakuwa kama lile tulilolizoea. lakini licha ya soka, sidhani kama maisha kwa ujumla wake yatakuwa sawa tena.

"Sisi wote tuna uzoefu kwamba kwa hali hii mambo yatabadilika na tutakumbuka namna ilivyotokea kwa namna moja au nyingine.

"Kwa upande wangu, nahisi huzuni hasa kwa wale waliopoteza ndugu zao kutokana na janga hili.

"Nina uhakika soka na michezo yote kwa ujumla itaathirika sana. Kifedha pia kutakuwa na tatizo, kwa sababu kuna kampuni ambazo zinahusika na michezo, hivyo kutakuwa na ugumu kutokana na mlipuko wa corona.

"Lakini pia binafsi kwa namna moja au nyingine naona hata kwenye mazoezi hali ni tofauti, kwani wachezaji watarudi uwanjani, lakini wakiwa hawana morali kubwa.

"Itakuwa hali tofauti kabisa na ngeni kwetu, na kwa uhakika kabisa soka halitakuwa tena kama lile tulilozoea."

## ZISIKUPITE

### BAYERN KWA SANE, KAI

BAYERN Munich inataka kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, 24, na kiungo wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz mwenye umri wa miaka 20, wote wakiwa wachezaji wa kimataifa wa Ujerumani - kama sehemu ya "zama mpya" klabuni hapo, amesema makamu mwenyekiti wa klabu hiyo. ***(Bayern 1, via Evening Standard)***

### ARSENAL 'YAIBIPU' NAPOLI

ARSENAL wana nafasi kubwa kumsajili mshambuliaji wa Napoli, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26 raia wa Poland, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Juventus. ***(La Repubblica, via Star)***

### WERNER AICHOSHA INTER

STRAIKA wa RB Leipzig na mchezaji anayetolewa macho na Liverpool, Tino Werner ameweka wazi uamuzi kuhusu mustakabali wake katika mazungumzo kuhusu uhamisho wake, na amueleza Mkurugenzi wa Michezo wa Inter Milan, Piero Ausilio. Ausilio amesema Mjerumani huyo mwenye umri wa miaka 24, "hatakuja kwetu". ***(Daily Star)***

### LUIZ KUONGEZEWA MKATABA

KLABU ya Arsenal inatarajia kukubali kuongeza mkataba wa beki wa kimataifa wa Brazil, David Luiz mwenye umri wa miaka 33, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo. ***(Evening Standard)***

### UNITED YAMSHTUKIA RAIOLA

MANCHESTER United inaamini wakala Mino Raiola ndio mtu pekee anayetaka Paul Pogba kuondoka katika klabu hiyo kipindi cha majira ya joto. Kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akihusishwa na Real Madrid na Juventus. ***(Times)***

### COUTINHO SOKONI BARCA

BARCELONA itatafuta pauni milioni tisa kama ada ya mkopo kutoka kwa klabu yoyote ya Ligi Kuu ya England kwa ajili ya kiungo wao, Philippe Coutinho. Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 27, ada yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 71. ***(Mundo Deportivo, via Mirror)***

### CAMAVINGA AZUIWA RENNES

RENNES imekataa kumuuza mchezaji wao anayewaniwa na Liverpool na Real Madrid, Eduardo Camavinga kipindi hiki cha majira ya joto. Mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21 mwenye miaka 17, pia amekuwa akihusishwa na Manchester United. ***(RTL, via Evening Standard)***

### CHELSEA MBELE KWA TELLES

CHELSEA inaiongoza Paris-St Germain katika mbio za kuwania kumnasa beki wa kushoto wa Porto na raia wa Brazil, Alex Telles, 27. ***(Tuttosport via Express)***

### OSIMHEN ANOGEWA EPL

LILLE wamepata ofa nyingi kwa ajili ya mshambuliaji wao Osimhen. Tottenham, Liverpool na Arsenal ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mchezaji huyo raia wa Nigeria mwenye umri wa miaka 21. ***(Daily Mail)***

### ELLIOT AIKATAA MADRID

KIUNGO wa kati wa Liverpool, Harvey Elliot, amekacha nafasi ya kujiunga na Real Madrid. Raia huyo wa Uingereza mwenye umri wa miaka 17, alikuwa amealikwa kukutana na Sergio Ramos katika jaribio la kumshawishi kujiunga na miamba hao. ***(The Athletic)***

HABARI MICHEZO

## Kahata afunguka 'ushikaji' wake na Kagere

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Mkenya Francis Kahata ameweka wazi urafiki wake na mshambuliaji kinara Meddie Kagere kuwa si wa leo wala jana kutokana na kufahamiana kwa muda mrefu kwa kucheza pamoja katika timu mbili tofauti kabla ya kukutana tena Msimbazi.

Kahata ambaye ametua nchini Jumamosi akitoka kwao Kenya, alipokuwa mapumzikoni kutokana na likizo iliyotokana na mlipuko wa virusi vya corona, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, alisema anamfahamu vema Kagere na ni rafiki yake mkubwa ndani na nje ya uwanja.

Alisema ni mshambuliaji hodari na ana matumaini makubwa na nyota huyo kuendelea kufunga kutokana na kasi yake uwanjani ambayo anaifahamu vema kutokana na kucheza pamoja timu tatu tofauti.

"Kagere ni mshambuliaji mzuri na anajua kutumia nafasi ipasavyo mimi naamini ataendelea kufanya vizuri na kuisaidia Simba, nimecheza naye timu mbili kabla ya kuja hapa Simba hivyo namjua vizuri," alisema Kahata.

Wawili hao walicheza pamoja katika timu ya KF Tirana ya Albania msimu wa 2014/15 kabla ya kukutana Gor Mahia ya Kenya na sasa Simba.

## Mwadui yaanza kuitisha Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Mwadui FC ya Shinyanga umeitaka Yanga kujiandaa kupokea kichapo watakaposhuka katika dimba la Kumbukumbu ya Kambarage mkoani Shinyanga Juni 13, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu kutoka Shinyanga, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Khalid Adam, alisema hawaihofii Yanga kutokana na kuwa wote wanashiriki Ligi Kuu.

"Yanga wajue hatutakubali kupoteza tukiwa kwetu, tumejipanga kwa muda mrefu kabla ya ratiba kutoka," alisema Adam.

Aidha, alisema lengo lao ni kushinda michezo yote ili washike nafasi nzuri, pamoja na kuendelea kushiriki Ligi Kuu msimu ujao.

"Sitaki kuwapa presha wachezaji wangu kuelekea katika mchezo huo tutaingia uwanjani na mfumo ule ule ambao tulikuwa tunautumia kabla ya Ligi Kuu kusimama," alisema Adam ambaye hadi ligi hiyo inasimama ameiwezesha timu hiyo kushika nafasi ya 12 kwenye msimamo ikiwa na pointi 34 zilizotokana na michezo 28.

Katika ratiba iliyotangazwa jana na Bodi ya Ligi (TPLB) kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu, Almas Kasongo, inaonyesha Yanga iliyopo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo ikiwa na alama 51 zilizotokana na mechi 27, itafungua ligi hiyo dhidi ya Mwadui FC Juni 13, mwaka huu, iliyokuwa imesimama kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

# MSIMU ALIA NA MSIMU MGUMU LIGI KUU Z'BAR

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa timu ya KMKM, Ame Msimu, amesema msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar, umekuwa mgumu zaidi kwa licha ya serikali kuchukua hatua ya kujikinga na ugonjwa wa Covid -19 tangu ulipoingia nchini na kusababisha kusimama kwa ligi hiyo ambayo kwa sasa imeruhusiwa kurejea.

Akizungumza na gazeti hili kocha huyo, alisema kwa sasa makocha watakuwa kwenye wakati mgumu kuweza kuwarejeshea wachezaji hamu ya kucheza mpira kutokana na kukaa muda mrefu bila kushuka dimbani ikilinganishwa na hapo awali.

**Alisema kwa upande wake na kikosi chake cha KMKM, atalazimika kuwapa wachezaji mazoezi ambayo hayatoleta athari pindi watakaposhuka dimbani kuendelea na ligi hiyo ambayo ilisimama kwa takriban miezi miwili sasa.**

Aidha, alisema matarajio yake makubwa ni kuona kikosi hicho kinafanya vizuri katika kumalizia michezo yake ili waweze kutetea ubingwa wao na kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunasubiri Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) kutoa mwongozo wa kufanya mazoezi ili kikosi chetu kiweze kujinoa kumalizia ligi japo malengo yetu hayatafikia kwa asilimia 100, lakini hata tukifia asilimia 90 kwetu ni mafanikio kutokana na kipindi hiki tulichopo," alisema.

KMKM ndiyo iliyopo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 46, huku nafasi ya pili ikishikiliwa na JKU ikiwa na pointi 45 na Mlande yenye alama 44, ipo nafasi ya tatu.

Ligi Kuu Zanzibar inatarajiwa kuanza kati Juni 16 ama 20, ikiwa ni baada ya Wizara ya Afya kuwapima wachezaji na kujiridhisha na afya zao, ili kuepuka maambukizo ya virusi vya corona ambavyo vinaendelea kuitesa dunia.

YAMETIMIA...




Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla (kushoto), akisaini mkataba wa ushirikiano na Kampuni ya LaLiga kupitia Klabu ya Sevilla ya Hispania juzi, usiku katika Hoteli ya Serena jijini Dares Salaam. Kulia ni Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Kampuni ya GSM wanaosimamia mchakato huo kwa gharama zao, Hersi Said na wanaoshuhudia ni wanasheria wa pande zote mbili (Yanga na GSM). **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Ruvu Shooting kuitibulia mazoezi Simba*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya ratiba ya Ligi Kuu inayotarajiwa kurejea Juni 13, mwaka huu kutoka na Simba kupangwa kuanza dhidi ya Ruvu Shooting, benchi la ufundi la mabingwa hao watetezi limesema litakutana kutazama namna ya kubadili programu ya mazoezi tayari kwa ajili ya kuivaa miamba hiyo ya Pwani.

Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), jana ilitangaza ratiba mpya ya ligi hiyo ambayo ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, ambapo sasa inarejea Juni 13 kutokana na serikali kujiridhisha na kushuka kwa maambukizo na wagonjwa waliokuwa hospitalini kupona.

Katika ratiba hiyo iliyotangazwa jana na Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almas Kasongo, Simba imepangwa kuanzia Uwanja wa Taifa Juni 14, mwaka huu dhidi ya Ruvu Shooting wakati Azam FC yenyewe ikiikaribisha Mbao FC kwenye dimba lao la Azam Complex, ikiwa ni siku moja baada ya Yanga kushuka katika dimba la Kambarage mjini Shinyanga kuvaana na Mwadui FC.

Ratiba hiyo itaendelea Juni 17, kwa JKT Tanzania kuialika Yanga katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma kabla ya Juni 20 wenyeji hao kuwaalika tena Singida United siku ambayo Ndanda FC nayo itakuwa mwenyeji wa Biashara United katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona.

Kadhalika, Namungo FC itaialika Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Majaliwa wakati Coastal Union ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar katika dimba la Mkwakwani mkoani Tanga wakati huo Polisi Tanzania ikiikaribisha Lipuli FC Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Mbeya City itakuwa mwenyeji wa Alliance katika Uwanja wao wa Kumbukumbu ya Sokoine, huku KMC ikiialika Ruvu Shooting kwenye dimba la Uhuru na Simba ikiikaribisha Mwadui FC katika Uwanja wa Taifa.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa klabu ya Simba, Patrick Rweyemamu, alisema hawezi kutolea ufafanuzi kuhusu mazoezi ya timu hiyo kwa sasa, mpaka watakapokutana na Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck, kujua mikakati mipya baada ya ratiba hiyo kuelekea kukutana Ruvu Shooting Juni 14, mwaka huu.

"Siwezi kuzungumzia ratiba mpaka nitakapokutana na benchi nzima la ufundi, huenda programu ikabadilika ndio naenda kukutana na kocha sasa hivi (jana mchana) kwa leo vuta subira," alisema Patrick.

Meneja huyo alisema wachezaji wanaendelea vizuri na mazoezi na kudai morali ya kila mchezaji ipo vizuri huku akieleza kuwa anashukuru tangu waanze mazoezi hawajapata mchezaji mgonjwa hata mmoja.

"Wachezaji wanaendelea vizuri hatuna majeruhi hata mmoja lengo ni kuendeleza ushindani na kubakiza kombe la ubingwa Msimbazi," alisema.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kuwapa sapoti kuelekea katika michezo iliyopo mbele yao.

# Michezo

Jumanne Juni 2, 2020

Nipashe





Messi atabiri soka tofauti la corona

UKURASA 22

NYONGA HIYO...




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Mkenya Francis Kahata, akifanya mazoezi ya viungo chini ya usimamizi wa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck. Kahata alichelewa kujiunga kambini na wenzake kutokana na karantini ya mlipuko wa virusi vya corona inayoendelea kwao, Kenya. **PICHA: SIMBA**

# Kikwete achambua mabadiliko Yanga

## ●●● Atamani haya ya ushirikiano na La Liga sasa yatimie, Msolla naye aeleza jinsi...

**Na Adam Fungamwango**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Kikwete, amechambua na kuelezea matumaini yake kuwa safari hii mabadiliko ya muundo mpya ya uendeshaji ndani ya klabu ya Yanga yatafanikiwa, baada ya kushindikana mara mbili huko nyuma.

**Kikwete ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya kutiliana saini kuanza safari ya mabadiliko kati ya Yanga na La Liga, chini ya udhamini wa Kampuni ya GSM, uliofanyika juzi usiku kwenye Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam, alisema anaamini safari hii yatafanikiwa kutokana na muda mrefu wa maandalizi ya kutosha kwa elimu itakayotolewa kwa wanachama na klabu hiyo.**

Kikwete alianza kwa kuchambua mabadiliko ya Yanga yalivyopitia vipindi tofauti kwa kueleza kuwa matamanio ya mabadiliko ya uendeshaji katika klabu ya Yanga ni ya muda mrefu na si ya leo, juzi.

"Mtakumbuka wakati wa Katibu Mkuu, George Mpondela 'Castro', akataka kuja na Yanga Kampuni, lilikuwa ni jaribio kubwa, la pili lilikuwa dhana ya kukodisha. mengine yalikuwa ni mabadiliko ya katiba tu," alielezea Kikwete ambaye ni mdau mkubwa wa soka nchini, huku akiongeza:

"Hili ni jaribio la tatu kubwa. Majaribio mawili makubwa hayakufanikiwa na kuleta mgawanyiko kwenye klabu. Ya Castro yalikuwa na Yanga Kampuni na Yanga Asili na yalileta vurumai kweli kweli, nia yake ilikuwa nzuri, ila wazo lake halikueleweka. Hata wazo la kukodisha nalo lilileta matatizo. Kuna waliotaka klabu ikodishwe na ambao hawakutaka hata kusikia."

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Mshindo Msolla, alisema baada ya kutiliana saini ya makubaliano ni hatua ya kwanza kuelekea kwenye mabadiliko ambayo ni ndoto ya muda mrefu.

"LaLiga anakuja kusaidia pale ambapo sisi tunahitaji atusaidie, siyo kutuelekeza tufanyeje.

"Mapendelezo ya kwanza tayari tulishapata kwenye Kamati ya Alex Mgongolwa, kikubwa wataamua watatusaidia njia ambayo sisi tunataka tupite kwa kutushauri tupite vipi, lakini maamuzi ya mwisho yatakuwa ni ya uongozi na wanachama wa Yanga," alisema Msolla.

Aliongeza kuwa kila kitu kitakuwa ni shirikishi hadi dakika za mwisho za mabadiliko.

"Hakuna mwekezaji atakayekuja kuwekeza kwenye klabu ambayo haiko sawasawa, au inadaiwa, hivyo awamu ya kwanza ni kuangalia muundo na kuboresha wanachama, nawashukuru GSM ambao wanataka Yanga ijitegemee," Mwenyekiti huyo alibainisha.

Kwa upande wa mwakilishi wa GSM, Injinia Hersi Said, alisema wanachohitaji wao ni kuacha alama na thamani ndani ya klabu hiyo kongwe nchini ili hata mwaka watakapoondoka, waache kumbukumbu kwa wanachama wa Yanga na vizazi vijavyo vya mashabiki wa soka nchini.

# Ni Simba na Ruvu, Yanga vs Mwadui

**Na Mwandishi Wetu**

KIPENGA cha Ligi Kuu kurejea rasmi dimbani kimepulizwa baada ya Bodi ya Ligi (TPLB), kutangaza ratiba ya mechi kwa kuanza na viporo Juni 13, 14 na 17, mwaka huu kabla ya siku tatu baadaye mtifuano huo kuendelea kwa timu zote kushuka viwanjani zikiwa zimecheza mechi sawa.

Katika ratiba iliyotolewa jana na TPLB kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu, Almas Kasongo, inaonyesha mabingwa watetezi, Simba watakuwa wenyeji wa Ruvu Shooting Juni 14 katika Uwanja wa Taifa ikiwa ni siku moja baada ya watani zao, Yanga kumenyana na Mwadui FC kwenye dimba la Kumbukumbu ya Kambarage mkoani Shinyanga.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Kasongo alisema mechi nyingine za viporo zitakuwa kati ya Coastal Union itakayoikaribisha Namungo FC katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga Juni 14 siku ambayo Azam FC watakuwa wenyeji wa Mbao FC kwenye Uwanja wa Azam Complex.

Alisema Juni 20 baada ya viporo hivyo kumalizika, JKT Tanzania watakuwa wenyeji wa Singida United siku ambayo Ndanda FC nayo itaialika Biashara United katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona, huku Namungo FC ikiikaribisha Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Majaliwa wakati Coastal Union ikiwa mwenyeji wa Mtibwa Sugar katika dimba la Mkwakwani mkoani Tanga na Polisi Tanzania ikiikaribisha Lipuli FC Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Kasongo alisema siku hiyo pia, Mbeya City itakuwa mwenyeji wa Alliance katika Uwanja wao wa Kumbukumbu ya Sokoine, huku KMC ikiialika Ruvu Shooting kwenye dimba la Uhuru na Simba ikiikaribisha Mwadui FC katika Uwanja wa Taifa.

Hadi ligi hiyo inasimama, mabingwa watetezi, Simba ndiyo waliopo kileleni wakiwa na alama 71 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 28, huku Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma ikishika nafasi ya tatu kwa pointi zake 51.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042